MUHTASARI WA KONGAMANO LA MWEZI
NJUWENI HOTEL - KIBAHA—5/3/1998

Kongamano lilipoanza wajumbe walikuwa wamejipanga kwenye meza mbili ndefu ambazo wajumbe wakikaa wanaangaliana.Upande mmoja wakakaa wajumbe wa upande wa Bakwata na upande mwengine wajumbe wa upande wa Ansaar Sunna.Sehemu ya meza kuu katikati ya ncha mbili za meza hizo walikaa sheikh mkuu,marehemu sheikh Hemed bin Jumaa bin Hemed na naibu mufti wa Zanzibar.

Katika wajumbe wa upande wa Bakwata kulikuwa na masheikh wengi wa kutoka Tanga.Baadhi ninaoweza kuwatambua ni sharifu Hussein Hashim,sheikh Mohammed Idi na marehemu skh Salim Kassim.

Masheikh wawili muhimu katika mjadala wa mwezi kutoka Tanga ambao wakazi wa Tanga wamezoea kupata hoja zao kupitia vipeperushi na vipaza sauti; hawakuwepo siku hiyo.Masheikh hao ni sheikh Salim Barahiyaan na sharifu Mohammed Yahya

Kongamano lilianza kwa msemaji kutoa ratiba ya shughuli za siku hiyo.baadae kikao kikafunguliwa rasmi kwa Qur'an tukufu ,surat Asr iliyosomwa na ustadh Muhidin.

Muongozaji kikao akasimama tena kumkaribisha marehemu sheikh mkuu,sheikh Hemed bin Jumaa ili atoe nasaha zake.

Katika kumkaribisha sheikh mkuu,mwongozaji kikao akamtambulisha sheikh mkuu kuwa mbele yake kulikuwa na viongozi wa Jamaatu Ansaar Sunna,ambao alisema ndio walioomba kupitia kwa makamo wa rais kukutana naye.Akasema vile vile mbele yake kulikuwa na maimamu kutoka misikiti ya sehemu mbali mbali nchini.

- **HOJA ZA BAKWATA**

MAREHEMU SHEIKH MKUU-HEMED BIN JUMAA BIN HEMED

Sheikh mkuu akaanza kwa dua ya ufunguzi,halafu akawashukuru wote wale waliokubali kuuitikia mwito wake ule, na hasa kwa kujihimu na kuwahi kwa vile mwaliko wenyewe alikuwa ameutoa muda mfupi tu.Akasema hakukuwa na wa kuwalipa asiyekuwa Mwenyezi Mungu subhaanahu wa taala.

Akasema, alipokuwa Tanga alipata wito wa makamu wa rais,marehemu Dkt Omar Ali Juma kuwa alikuwa amepokea ombi kutoka kwa vijana wake wanaoitwa Ansaar Sunna,ambao walitaka waonane na yeye.

Sheikh mkuu akatoa matumaini kwa vijana wake,kuwa watakaposimama wangetoa sababu yao,ya wao kujiita Ansaaru Sunna badala ya Ansaaru Llaah kama ilivyo kwenye Qur'an,aya ya 14 ya Surat Saff (61).Kama sababu zao zikiwa na uzito basi Bakwata wangewafuata wao,na kama ni kinyume chake basi wote wawe ni Ansaaru Llaah.

Salamu hizo ilikuwa ni salamu nzuri kwake,kwani kabla ya hapo salamu ambazo alikuwa ikizipata ni za matusi tu kupitia kwa ndugu zake ambao wanakaa jirani kabisa na msikiti wa jamaa wa Ansaar Sunna pale Tanga. Kama nilivyosema mwanzo, kuwa leo nimeitwa kwa furaha ili tuzungumze,hivyo mimi nimewasamehe kwa hizo salamu zao za matusi.Kwanza sijui kama ni kweli.Nimeona dalili tu za ukweli kwa salamu za khalati zangu hao wanaokaa jirani.

Makamo wa rais akasema alimtaka asisite kuonana nao.Aliarifiwa kuwa vijana hao walipenda kuonana naye,lakini hata kama asingesisitizwa kwa vile walipenda kuonana naye basi asingesita kuonana nao.Jambo hili wala halimuhusu yeye peke yake na jamaa wa Ansaar Sunna tu.Kama ni mushkeli basi umeenea ulimwengu mzima wa kiislamu

Vikao kama vile akasema vimefanyika Zanzibar,vimefanyika Kenya na kwengineko,na hata Saudia kwenyewe na maandiko yake anayo ambayo bado yanahitaji….(*hakumalizia kauli yake)*

Jambo la msingi alilotakiwa kuzungumza ni juu ya kuandama kwa mwezi wa Ramadhani na mfunguo mosi,jambo ambalo limeleta fujo na matatizo mengi.Akauliza jee katika misingi ya kisheria za kiislamu mwezi ukionekana Saudia ndio watu wote wanapaswa kufunga?.

Kwa hadithi ya Mtume صلى الله عليه و سلم ***swuumuu liru'yatih wa afttiruu li ru'yatih*** ndio watu wa ulimwengu mzima wanatakiwa wafunge ukionekana Saudia,kwa sababu tu haikusemwa ***swuumuu idhaa ra'aitumuh wa afttiruu idhaa ra'aitumuh*.**Lakini kwa hadithi hiyo hiyo sahihi mwezi ukionekana Thailand,Maskat au Yemen iliyopakana na Saudia basi haifai kwa Saudia kufunga na kwa waislamu wa ulimwengu mzima kufuata. Akashangaa sheikh Hemed.

Msingi wa hoja za wale wanosisitiza kufuata mwezi wa Saudia ni kuwa Mtume صلى الله عليه و سلم kazaliwa Makka,lakini ikumbukwe kuwa Makka hiyo hiyo ndiyo iliyomfukuza Makka akahamia Madina na kufia Madina.Hoja nyengine ni kuwa Alkaaba iko Makka na waislamu wa ulimwengu mzima wakiswali wanaelekea huko.

Wanaosimamia hoja hiyo wanasema siku ya Arafa pia mahujaji wa kutoka ulimwengu mzima husimama Arafa iliyoko Makka.na kwamba mahujaji wakisimama Arafa wengine wanatakiwa wafunge siku ambayo ni suna muhimu Mtume صلى الله عليه و سلم aliyosema inafuta madhambi ya mwaka uliopita na mwaka ujao

Madai mengine ni kuwa saa zilizoko Makka ni sawa na saa za Tanzania.Sasa jee hiyo ndiyo sahihi ilhali watu walioko Saudia wakiswali adhuhuri kwa wengine ni usiku?,au sahihi ni kuwa kila watu wafuate matlai yao?.

Sheikh mkuu akawaomba wote waliofika hapo,Ansaaru Llaah na Ansaaru Sunna ikifika mwisho waafikiane ili wawe ni wamoja kwani inayotafutwa ni haki na wala si kufarikiana.Ikiwa ni sahihi kuwa ukionekana Saudia basi sote tufunge mapema pamoja,au ikiwa sahihi ni kuwa watu wa Makka wakiuona watafunga wao na wengine wasubiri wauone kwao,nitawaomba ndugu zetu wakubali kuwasubiri ndugu zao wa Ansaaru Llaah.

Ikiwa tumewashinda mutufuate,na ikiwa mumetushinda tuwafuate.Vyenginevyo ikifika pahali aah! hatukubali basi itakuwa ni kupoteza gharama bure.Isiwe tunazungumza jambo hilo kwa hilo bila kuafikiana,au ikawa tunaafikiana halafu hatutekelezi.Ikiwa hivyo ndivyo itakavyokuwa nitawaomba ndugu zetu wa Ansaar Sunna waturudishie gharama zetu.

Baada ya hapo ikasomwa dua na wajumbe wakachawanyika kwa chai na mapumziko mafupi na kurudi kikaoni.

Kabla kukaribishwa wazungumzaji kuanza mjadala rasmi,yakasomwa masharti ya ziada ya kongamano na mmoja ya masheikh upande wa Bakwata.Kwanza si ruhusa kwa sheikh yeyote aliyetoka nje ya Tanzania kuchangia chochote.Wao kama wapo wangeruhusiwa kuwa wasikilizaji tu.

Kile hakikuwa kikao cha mashindano,bali ni cha kutafuta hoja tu kwa maslahi ya umma wa kiislamu.

Waandishi wa habari wote wa magazeti na vyombo vyengine vya habari hawakuruhusiwa kuwepo ndani ya kikao kile.Wasije wakachanganyikiwa na kuandika mambo yasiyohusiana na madhumuni yaliyokusudiwa.Kwa kweli wala hawakualikwa kwa

makusudi mazima,wao wenyewe tu wamefika,na si jambo baya ,lakini hawaruhisiwi kubaki ndani ya kikao.Waliokaidi kutoka nguvu zikatumika kuwatoa.

Ikaelezwa kuwa waandishi wa habari wangepewa taarifa ya kilichokubaliwa mwisho wa shughuli yote.

Ilitakiwa achaguliwe mwenyekiti wa kikako ambaye asingekuwa na upande wowote kati ya pande mbili zilizofika kushiriki.Hata hivyo waandaaji wa kongamano kwa kushauruiana pande zote, siku chache kabla ya siku hiyo,walihisi isingewezekana kumpata mtu wa aina hiyo,hivyo wakakubaliana wamchague mmoja wao ambaye angeweza kuuficha upande wake.Upande wa Bakwata waliyemuona angefaa kwa sifa hizo ni sheikh Issa Shaaban Simba,sheikh mkuu wa mkoa wa Shinyanga.Muongozaji wa kikao akamuombea dua kwa Mwenyezi Mungu ili aweze kuendesha shughuli ile kwa ufanisi na uadilifu.

Yakasomwa majina ya masheikh 10 wa Ansaar Sunna ambao waliorodheshwa kuchangia hoja.Ikaelezwa kuwa masheikh watatu kati yao hawakuweza kufika, ambao ni sheikh Salim Barhiyaan,sheikh Juma Poli na sheikh Salim Rajab Sima.Pamoja na majina kumi ya upande ulioitwa wa Ansaaru Llaah,orodha ikakabidhiwa kwa mwenyekiti.

Akasimama skh Yussuf Rajab Mlenge upande wa Ansaar Sunna, akalalamikia utaratibu wa uenyekiti,akasema kwa uzoefu wake wa vikao kama hivyo anapendekeza pawe na wenyeviti wawili na makatibu wawili ili kuondoa shubha..Akasimama mwenzake mmoja kusaidia kufafanua hoja yake na kutia nguvu.Akasema vyenginevyo ni bora kuwe na wenyeviti watakaopokezana.Sheikh Ahmad Zubeir upande wa Bakwata akauliza kwani utaratibu ule una shaka gani ?.

- **HOJA ZA ANSAAR SUNNA**

SHEIKH SALIM MSABAH

Baada ya majadiliano marefu utaratibu wa uenyekiti wa kupokezana ukakubaliwa na ilipofika saa sita kasorobo mjadala ukaanza.Akasimama sheikh Salim Msabah kusoma alilioliita tamko la Jamaatu Ansaar Sunna.

Kabla kusoma tamko hilo akatumia dakika chache kujibu changamoto ya skh Hemed kuhusu jina la Ansaar.Akasema maana ya Ansaaru Llaah iliyo kwenye surat Swaff 61:14 inafasiriwa na Qur'an yenyewe kwenye surat Al Imraan 3:52

Ansaaru Llaah kwenye Qur'an 61:14 ni wale waliomnusuru Issa bin Mariam,kwa sababu Mwenyezi Mungu hana haja na nusra ya binadamu.Kwa upande wa nabii Muhammad ,Ansaaru Llaah ni wale wanaonusuru sunna za Mtume ﷺ , kwa sababu Mtume ﷺ hayupo,suna zake ndizo zinazomuwakilisha.

Mtu maarufu anayeitwa Ansaaru Sunna ni imamu Shaafi,kwani katika kitabu chake **Al Risala** ameitwa **Nasru Sunna** kwa umoja wake.Wakiwa wengi ni Ansaaru Sunna.

Jamaatu Ansaaru Sunna imepokea kwa mshangao mkubwa tamko la sheikh Hemed bin Juma bin Hemed alilolitoa kwenye Idul Fitri tarehe 30.01.1998.Tamko lilikuwa na nia ya kuwazuia waislamu wanaofunga na kula Idi kwa kufuata mwandamo wa kimataifa.

Kwa tamko lake hilo,baraza la ulamaa la Jamaatu Ansaaru Sunna lilikaa kujadili kwa kina athari zake kwa mwenendo wa Ansaaru Sunna kwa Tanzania.Kikao kiliamua utolewe ufafanuzi juu ya hoja zetu,ili atakae ongoka,aongoke juu ya hoja, na atakaepotoka apotoke juu ya hoja.Angalia Qur'an 8:42.

Jawabu zetu zimejengeka juu ya utafiti ndani ya Qur'an,katika suna za bwana Mtume ﷺ ,juu ya ijmainh ,qiyaas na utafiti wa kisayansi.Msimamo wetu ndio msimamo wa maimamu

wanne katika fiqhi mpaka kufariki kwao.Kauli zao zimeegemea kwenye aya ya 185 ya surat Al baqara.

Mwezi wa Ramadhani unaingia kwa kuandama mwezi popote ulimwenguni.Ilivyokuja kwenye Qur'an hakuna ufafanuzi wala msharti yoyote.Neno as-shaharu kwenye Qur.2:185 limetumika kwa maana ya mwezi wa Ramadhani.Angalia hayo kwenye **A**l **Mughniy** ya Ibnu Qudama, juzuu ya 4,uk 88-89.Ufafanuzi zaidi uko kwenye fatwa ya 760 kitabu cha ***Fatawa Al islaamia*** ,juzuu ya 5 uk 1747,kutokana na fatwa za wanavyuoni wa kimisri kilichotolewa na Daarul Iftah.

Kwa upande wetu Ansaaru Sunna;hakuna maandishi yoyote yenye kuonesha kuwa sisi tunafunga kwa kufuata Saudi Arabia.Mufti itakuwa amepotoshwa.

Sheikh Kassim Abul ghaith wa Lebanon kasema ukionekana mwezi katika nchi fulani itawalazimu na waislamu wa nchi nyengine .Hakuna tafauti baina ya nchi madam zimewafikia habari na wakawa wako katika usiku,kabla mapambazuko ya alfajiri.Hii inaendana na hadithi ya Mtume isemayo *Swuumuu liru'yatih*…...Pia inaendana na matakwa ya kisasa, kwa vile redio,magazeti,televisheni na simu vinawezesha kupata habari hizo kirahisi.Watu wa mashariki ya mbali wanaweza wakapata habari kutoka kwa ndugu zao popote na wakapatana katika kufunga kwao.Maelezo hayo yamo kwenye kitabu cha ***Mukhtariyaat mina Sunna*** cha skh Al Rafii uk.277-278.

Katika mwaka 1415 H sawa na mwaka 1994,skh Abdul Aziz bin Baaz,mufti wa Saudi Arabia alitoa fatwa kuwa kilicho sahihi ni kutofuata tofauti za machomozo ya jua ,yaani mattaali'i.Hiyo iko kwenye kitabu cha fatawa zake uk 208-216.

Kuhusu hadithi ya Kuraib,wanachuoni wengi wamekubaliana kuwa ina maana nyingi.Ibnu Qudama anasema alipokataa Ibnu Abbas kufuata habari ya Kuraib inaweza ikawa na maana ya kuwa alikataa kwa vile ushahidi wa mtu mmoja katika kufungua haukubaliwi,ila kwenye kufunga.

Azimio la Rabittatul Aalamul Islam alilolitaja skh Hemed,wanazuoni wengi walikubaliana kuwa mwezi ukionekana popote waislamu wengine wafuate.Ni kweli alitokea mwanachuoni skh Abdullah bin Hamed akapinga.Yeye mufti Hemed bin Jumaa ana haki ya kumfuata huyo mmoja mpaka hapo atakapopata hoja zilizo kinyume chake.Lakini jee haki ya kuwazuia wengine kuwafuata walio wengi kaipata wapi?.Ni yupi wa kushutumiwa na kukejeliwa,ni yule aliyemfuata mmoja au aliyewafuata walio wengi?.Ni kundi lipi kati ya haya mawili lenye kustahili kupata amani?;Qur'an 6:81.

Madai ya mufti kuwa maimamu wanne wametoa maamuzi bila kuiona riwaya ya Kuraib,ni madai ambayo twaamini kayatoa bila kuyafanyia utafiti.Habari ya maafikiano ya maimamu hao yanapatikana kwenye **Quttuufu Rabaaniy**,musnad wa imamu Ahmad bin Hambali jz 9,uk 270.

Ikiambiwa kila nchi na mwezi wake,inafaa tuthibitishiwe ni nchi ipi inayokusudiwa.Kwa sababu nchi kama Kongo au Sudan zina ukubwa kuliko nchi zote za Afrika Mashariki.Kwa kuangalia nchi ndogo kama Kuwait na Bahrain ina maana suala la masafa ni jambo lisilowezekana.Ikiwa ni suala la mamlaka mbona tunapokea habari kutoka Uganda au Kenya.

Ikiwa ni mattlai tuwekeeni wazi ni umbali kiasi gani,kwani matlai ya Dar es Salaam na Kigoma ni tofauti kwa zaidi ya nusu saa.Sasa jee kwanini watu wa Kigoma wafuate watu wa Dar es Salaam na wawache kufuata ndugu zao wa Rwanda na Burundi?.Kwa kufuata tafsiri za matlai Tanzania itakuwa na Idi zaidi ya 3,kwa sababu zipo sehemu huuona mwezi

baada ya siku mbili baada ya mwezi wa Bakwata.Kwa hali hiyo sisi tumeona ni aula kuacha kufuata kauli ambayo hatuna uhakika wake na haieleweki.

Mwandamo mmoja unathibitishwa na maendeleo ya kisasa ya kisayansi.Siku mahujaji wakiwa Arafa,watu wote wanaweza kujua kuwa kwetu sisi mchana wetu ni mmoja.Kukubaliana na Bakwata ni kuwanyima waislamu fadhila za siku ya Arafa.

Mwezi ukifika Lailatul badri,yaani siku ya 14,duara la mwezi huonekana ni kubwa kuonesha kwamba mwezi uliotangazwa na Bakwata uko nyuma,na ule tuliotangaza sisi unakubaliana nao.

Kusema kuwa uamuzi wa mufti ni wa mwisho kwa waislamu wa Tanzania ni kwenda kinyume na mafundisho ya kisheria ya kiislamu,bali ni kwenda kinyume na katiba ya Bakwata yenyewe;ibara ya 88 vifungu vidogo vya 2 na 3, vinavyoeleza kuwa asiyeridhika na fatwa ya mufti anaweza kutafuta fatwa kwengine.

Mpaka sasa kwa maelezo hayo hakuna sheria ya dini yetu, wala ya nchi tuliyoivunja ,hivyo hakuna haki ya kuzuiwa kutekeleza wajibu wetu.

- HOJA ZA BAKWATA
  SKH AHMAD ZUBEIR

Aliyefuatia ni skh Ahmad Zubeir wa upande wa Bakwata uliopendelea jina la Ansaaru Llaah.

Akasema anapinga kwa nguvu zote kuwa kuna miandamo tofauti ya mwezi;wa kimataifa na wa kitaifa Katika uislamu hakuna muislamu nambari moja na muislamu nambari mbili.Akatoa mfano wa Malkia Bilqis kama ilivyokuja katika Qur'an 27:44.Pamoja na ugeni wake katika uislamu,malkia Bilqis alitumia tamko la ***aslamtu ma'a Sulaimaan*** badala ya ***aslamtu bi Sulaimaan***,kuonesha kuwa yeye sasa katika uislamu ni sawa na Sulaiman (a.s) mbele ya Mwenyezi Mungu.

Madam wewe ume *surrender* kwa Mwenyezi Mungu,wewe ni sawa na mwarabu,ni sawa na mzungu na mtu mwengine yoyote.

Baada ya tamko hilo akasahihisha matamshi ya kilugha kuhusiana na Ibnu Qudama ilivyotamkwa na msemaji wa Ansaaru Sunna,Akasema ilivyo sahihi ni Ibnu Qudaama.

Mambo haya ya mwezi yanahitaji mazingatio.Nitaeleza wanavyosema ***usuulul fiqhi***.akina Al Aamidy na wengineo, kwenye juzuu inayoitwa ***Al maqaasid***.Anasema kaaida anazozileta Mwenyezi Mungu ni lazima ziwe ziko wazi,zimedhibitika na zinaenea kwa walimwengu wote.

Utakuta Mwenyezi Mungu alipozileta na kutufundisha nyakati za ibada ziko wazi na hazina matatizo.Kwa mfano tunapokuja kwenye swala katwambia kwenye Qur'an 11:114, kiasi kwamba hata aliye jaahili akielekezwa kidogo tu ataweza kufuata.Atafahamu wakati gani aswali magharibi ,wakati gani Isha na kadhalika.

Nyakati za swala zimewekwa kwa harakati za jua,kwa sababu swala ni ibada za kila siku.Sisi tuna miaka ya namna mbili,ya kimwezi na miaka ya jua.Mwenyezi Mungu alipotuletea swala,katuletea kwa miaka ya jua-***masiiru shams***.Ama ibada ya funga na hija,hususan swaumu ya Ramadhani,hii haifungamani na siku,bali inafungamana na mwezi.

Kwenye hija Mwenyezi Mungu kasema ***Al haju ash- hur***...,na kwenye Ramadhani katumia ***shahru Ramadhaan***...*H*aya ndiyo yale yale aliyosema Mwenyezi Mungu katika Qur'an 2:185.Oneni tofauti hiyo kati ya ibada ya swala na swaumu.

Ndugu zangu!, katika aya hatuna aya dhaifu na sahihi,aya hiyo nyote munaikubali.Kama aya hii ni ya umuumi,kwanini Mwenyezi Mungu asiseme ***faswuumuhu*** na akatumia ***fa***

lyaswumhu.Hii kama nilivyosema kabla, kwenye Al maqaasid,kuwa ni kwa vile sharia ni kitu chepesi.Mwenyezi Mungu hakujaalia dini kuwa ni jambo zito.Imeletwa jambo hili la kufunga kiasi kwamba asipate tabu mtu wa kijijini wala wa mjini.Wazee wetu vijijini wanaweka vijiti kwenye uzi ikifika 29 au 30 wanafunga.
Maelezo zaidi juu ya haya nenda kwenye ***Al Manaar***.Ikiwa kwenye **Al Fatawa** kuna maneno ya Muhammed Abduh.basi maneno yake hayawezi kuwa na nguvu kuliko kwenye tafsir yake ya **Al Manaar**.

Kuhusu fatwa, skh Tantawiy kasema katika jarida la **Manaar** akisherehesha hadithi ya Mtume صلى الله عليه و سلم ,kuwa watu wakiuona mwezi wafunge na ni juu ya wale ambao hawajauona wasubiri.Njia za kuuona mwezi ni tatu,kuuona kwa macho ,kukamilika Shaaban siku 30 au kuukisia mwezi.Ndipo pale Mtume صلى الله عليه و سلم swalla aliposema ***fain ghumma***.Kwa hivyo inaonesha tunakubaliana kuhusu ***manttuq*i** ya hadithi lakini tunakosana kwenye ***maf huum*** ya hadithi.Jee ni nani atakayekuwa ni jaji katika jambo hili?.

Kuhusu kuuona mwezi,sharia inasema ikiwa mimi nimeuona mwezi ni juu yangu kufunga lakini si juu yangu kuutangaza,isipokuwa niende kwa ***waliul amr***,yeye ndiye mwenye amri ya kuutangaza ule mwezi.

Arafa ndio siku pekee ambayo ni tofauti na siku nyengine.Siku zote huingia usiku lakini Arafa huingia baada ya kupambazukiwa na asubuhi.Sasa jee atakayefunga siku ya Arafa yule aliyeko Arafa atakuwa ameshawajibikiwa na Arafa?.

- HOJA ZA BAKWATA
  SHARIF MUHAMMAD YAHYA

Kwa heshima ya mshiriki maarufu wa mjadala wa mwezi wa jijini Tanga zifuatazo ni hoja zake kama alivyozitowa kwenye kipeperushi chake cha tarehe 20/08/2008 na kukikabidhi kwangu.

MWEZI MTUKUFU WA RAMADHANI UNAWADIA
MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. <u>WAJIBU WAKE</u>.

Hapana shaka sote twajua kuwa tumefaradhishiwa kufunga kwa kauli yake Allah (SW).

- Enyi ambao mumeamini! Mumewajibishiwa Saumu (kufunga) kama walivyowajibishiwa waliokuwa kabla yenu kwa ajili mupate kujihifadhi (na maovu)
- Katika siku maalumu (siku chache tu).....
- Ni mwezi wa Ramadhani ulioteremshiwa Quran yenye kuwaongoa watu na yenye dalili zilizowazi za uongofu na upambanuzi (wa haki na batili).....

Utayakuta hayo na zaidi kuhusu SAUMU katika Suratul Baqara kuanzia aya ya 183- 188.

2. **<u>KUINGIA KWAKE</u>**

Haingii Ramadhani ila kwa kuonekana mwezi au kukamilika Shaabani siku 30(thelathini). Hili nalo ni kwa maneno ya Mtume (S.A.W) “Msifunge mpaka muuone mwezi na msifungue mpaka muuone”

<u>KUMBUKA NA UZINGATIE TENA SANA</u>

Tunalazimika kutafuta na kuona mwezi kwani ibada zetu mbili zinazofungamana na kuonekana mwezi tena ni NGUZO MBILI kati ya tano za uislamu sasa zinavurugika kutokana na wasiotazama mwezi kuwa na mvuto mkubwa.
Kwa mfano: Hija iliyopita "Arafa" ilisimamiwa siku sio kutokana na SAUDIA kuuanza Dhul Hija kimakosa kama walivyothibitisha wao wenyewe baadae kwa kuufanya mwezi uwe na siku 31 (thelathini na moja)!
Ramadhani kadhaa zimeanzwa sivyo na kumalizwa sivyo na wengine kulipa yote kwa kutozingatia kuangalia mwezi na kwa kufuata matangazo tu.

MATARAJIO YA MWEZI MTUKUFU WA RAMADHANI 1429 H

Kwanza kabisa tujue kuwa huu mwezi wa Shaabani kuna waliouanza Jumamosi AUGUST 2 Jumapili AUGUS 3 na Jumatatu AUGUST 4. tofauti duniani hiyo.

UTAMALIZIKAJE?

Jumamosi AUGUST 30/2/2008 saa 4:58 usiku kwa saa zetu (19.58 GMT) mwezi unaingia mafichoni (kuzaliwa Astronomical New/Moon). Hauonekani popote duniani yaani hata kwa wale ambao kwao ni mchana wakati huo wafikapo jioni hawataona.
Kwa mujibu wa wanataaluma AUGUST 31/2008 Jumapili unaweza kuonekana Amerika ya kusini kwa jicho na labda Afrika ya Kusini na Amerika ya kati, kama hali itakuwa nzuri. Itakuwa vigumu kuonekana mwezi Amerika ya kaskazini AUG 31 lakini utaonekana sept 1 Inshaalah. Kwa hivyo
Ramadhani 1 Amerika ya kaskazini kwa mujibu wa kuonekan mwezi yatarajiwa kuwa sept 2 Inshallah.
Hata hivyo kwa mujibu wa SAUDI UMMUL – QURA KALENDAR, BARAZA LA FIQH LA MAREKANI YA KASKAZINI NA BARAZA LA ULAYA LA FATWA NA UTAFIT.Hao siku yao ya kwanza itakuwa Jumatatu septembe 1.
(BILA KUONEKANA MWEZI HUKO KWAO)

Uingereza mwezi utakuwa bado hauonekani Sept 1. hata hivyo kwa mujibu wa FATWA MPYA YA DEOBAND INDIA siku ya kwanza ya Ramadhani Uingereza itakuwa septemer 2 kwa sababu mwezi utaonekan kirahisi kwa jicho kunzia Australia mpaka Morocco (tukiwamo Tanzania). Pakistani nao wataangalia mwezi sept 1 (kumbuka kwao hiyo ni 29 shaabani) Ramadhani itaanza Sept 2
MWISHO
Tumetoa taarifa hii kwa urefu ili kuonyesha umuhimu wa kuangalia mwezi na kuthibitisha kuwa kuna wasioangalia mwezi na kuwa hakujawa na Ramadhani moja siku zote hizi na kwamba pia si kweli kuwa mwezi waonekana kwanza mashariki ya Kati kama wanavyolazimisha wengine.
TUMCHENI ALLAH (S.W)

MWENYEZI MUNGU ATUJAALIE RAMADHANI YENYE
KHERI NA BARAKA

WASALAAM

KHERI KUBWA ITAPATIKANA INSHAALLAH.

MUHAMMAD SHARIF YAHYA ALBAARY
TANGA.
18 SHAABAN 1429H
20 AUGUST 2008 M

- **HOJA ZA ANSAAR SUNNA**
  SHEIKH JABIR KATURA

Msemaji wa pili upande wa Ansaar alikuwa ni skh Jaabir Katura.Kwanza akakosoa matamshi ya kilugha ya msemaji aliyemtangulia.Moja ya aina ya swaumu aliyoitaja ilikuwa ni matusi,akasema hakuna swaumu hiyo.

Si kweli kuwa Allah (s.w) amefungamanisha swaumu na mwezi,na swala kwa jua.Uhakika ni kuwa swaumu imefungamanishwa na siku,Qur'an 2:184.Mwezi ni sababu ya kupatikana siku za mwaka na siku za mwezi na hisabu.Katika Qur'an ni ***Adaada siniina wal hisaab*** Qur'an 10:5 na 17:12.Haikutajwa ***adaada saat*** amabayo ndiyo ingekuwa ya jua .

Man shahida minkum,haina maana kuwa kila mmoja lazima auone kama alivyosema mwenzetu sheikh Zubeir.Yeye katwambia kuwa sisi tuko kwenye makosa kumbe yeye yuko kwenye makosa makubwa zaidi na ya ajabu.Kwa msisitizo akasema;Tutamtaka aje tena kutueleza hiyo mipaka ya **mattaali'i** ni ipi hasa anayoikusudia ?.

Sisi sio tuliosema hayo.Mwanachuoni mkubwa na imamu wa Al Azhar sheikh Ally Jaadul Haq, kasema mmoja akiuona mwezi basi hukumu yake huenea kwa wengine.Kuonekana mwezi ndio asili na hakuna matlai.

Watu wa miji na maeneo tofauti wakishirikiana usiku hata ukiwa kwa masaa machache basi watashirikiana kwa ibada zao kama funga.Hii anasema inaendana na lengo lililokusudiwa na uislamu katika kuwaunganisha waislamu wa miji mbali mbali.Miji iliyokusudiwa ni miji ya kiislamu na sio nchi zilizogawanywa na wakoloni.

Kuhusu Arafa imelazimika kwa matlai ya Makka;mji mtukufu.Kwa hivyo ikiwa ni matlai inabidi waislamu wote wafuate matlai ya Makka.Arafa haiwi ila siku ya 9 ya Dhul Hijja.Haijuzu kuhitilafiana siku hiyo baina ya mji mmoja na mwengine.Haiwezekani kuwa mahujaji wa Tanzania leo wako Arafa lakini huku nyumbani waje wafunge kesho kuwa ndiyo Arafa.

Kwa kifupi siku ya Arafa ni siku mahujaji wanaposimama Arafa,vyenginevyo siku hiyo itapoteza maana yake.Ikiwa Hajj mwenyewe hawezi kuilipa siku hiyo huku yuko Makka,pindi akipatwa na dharura kama maradhi na akakosa mtu wa kumpeleka Arafa.Itabidi afunge safari tena upya.Itakuwaje mtu mwengine anayeitakidi kuwa Arafa ni siku nyengine kabisa !.

Wenye mamlaka,waliopewa majukumu ya kusimamia mambo ya waislamu ni juu yao kufanya utafiti wa kihakika kwa miezi miandamo tangu Muharram mpaka Dhul Hijja,na sio kukaa kusikiliza tu.

Hakuna makosa kwa mtu kusaidia katika njia za kielimu na kiteknolojia zilizoenea ili kuwafanya watu wasipishane kwenye ibada zao za funga na Hija.***Wabillaahi Tawfiiq***.

- **HOJA ZA BAKWATA**

Skh AHMAD ZUBEIR

Mwenyekiti,skh Issa Shaaban akatoa nafasi tena kwa sheikh Ahmad Zubeir aliyekuwa na shauku kutetea hoja zake kutokana na changamoto ya sheikh Jabir Katura.

Sheikh Ahmed Zubeir akaanza kwa kusema kuwa amefurahi sana na majibu ya kaka yake skh Jaabir Katura, halafu akaendelea kwa kujigamba kwamba;Ndugu yangu sheikh Jabir kasema sana,lakini mpaka sasa bado hajajibu hoja yangu.Kiti changu hiki nilichokalia mpaka sasa sijaondolewa,aje mtu aniondoe !.

Tumesema kwamba sisi sote tunakubaliana katika **nusus** lakini tunatafautiana katika **mafhuum** ya hadithi.Nimependelea kumtaja aliyekuwa mufti,ambaye sasa ni **sheikhul Az har,s**heikh Muhammed Said Tantawiy.Katika kuieleza hadithi kasema ni juu ya wale ambao hawajauona mwezi kusubiri.Aliyoyaeleza sheikh hapo ni **mafhuum** tu.

Ukija huku yuko Al Iqrima na wenzake wanasema hivi na hivi !.Sasa jee ni nani ambaye katika nchi ni hoja wa kuyaondoa haya?.Ni ***waliul amr***.Haiwezekani hawa kufunga leo hawa kesho.Au hawa kula idi leo na wengine kesho. Hili halikubaliki katika nchi yoyote **Waliul amr** wetu akisema fuateni China ***fa ahlan wa sahlan***.

Hapo nimeona kitabu cha Qardhawiy,fungueni mutaona hayo.Mimi sikujitayarisha vya kutosha lakini ningeleta dalili nyingi tu juu ya hilo.

Baada kusema hivyo mwenzake akamletea kitabu alichokifungua tayari ukurasa husika, ili asome,hata hivyo hakukisoma.Wakati huo kulikuwa na mikono upande wa pili waliotaka wachangie papo kwa papo.

- **HOJA ZA BAKWATA**
  SHEIKH MUHAMMED IDD

Kabla kuanza kutoa hoja zake akamuomba mwenyekiti kuendelea kuuacha wazi mlango wa kukosoana kilugha pamoja na kwamba sheikh wetu Jaabir Katura hakuupendelea, kwani kosa dogo katika lugha ya kiarabu hubadili maana pakubwa.Kukosoana ni jambo la kidini na halina matatizo.Kwenye hadithi moja ya Mtume صلى الله عليه و سلم kasema ikihudhuria **as-shaa** na **ishau**,basi mtu kwanza atangulize **as-shaa** kabla ya **ishau.**Fikiria pahala pa **as-shaa** ukaondoa ukaweka **ishau**.

Ndugu zangu skh Salim Msabah na skh Jaabir Katura wamezungumza sana.Kwa upande wa skh Salim Msabah yeye kataja pande zote,zinazoegemea **ikhtilaaful mattaali'i** na zisizoegemea,lakini kaupa nguvu zaidi upande usioegemea.Sheikh Jaabir yeye kataja pande hizo lakini hakutaja kabisa hoja za wanaofuata **ikhtilaaful mattaali'i**,kama kwamba upande huu hauna hoja,kumbe zipo na ni madhubuti.

Ili isije jengeka dhana kwa wasikilizaji na watazamaji watakaoziangalia kaseti hizi,nitatoa hoja na kuzitetea kutia nguvu upande wetu.Nitaomba ufunguliwe mlango mwengine ili nimuhoji sheikh Jaabir Katura kuhusu hoja alizozitoa,na yeye anihoji kuhusu hoja zangu.

Ndugu waislamu,jambo hili la kukhitilafiana kwa machimbuko ni jambo lipo.Tuanzie na mwanawachuoni Said Omar Albarakaat.Huyu ni mtungaji wa kitabu cha ***Faidhul Ilaah Maalik*** kwenye ukurasa wa 273.Katika kuthibitisha kuwa **ikhtilaaful mattaali'i** iko anasema maneno haya:Ukionekana mwezi kwenye mji mmoja kinyume na mji mwengine basi pana upambanuzi.Upambanuzi wenyewe ni kukhitilafiana miji hiyo kwa kukhitilafiana machimbuko yao kama vile Hijaz na Iraq au Misri na Khurasan.Kukosa kukhitilafiana ni kwa kuwa na matlai mamoja kama vile Kufa na Baghdad..

Miji ikikurubiana basi hukumu ya mwezi huenea baina yao.Na ikiwa haikukurubiana basi hukumu hainei baina ya miji hiyo.Mji ambao uko mbali na mji uliouna mwezi haiwalazimu kufunga.Mwanachuoni huyu ametolea dalili maelezo yake kwa hadithi ya Kuraib.Hadithi hii iko kwa urefu kwenye shereh ya **Sahihu Muslim** jz 7 uk.167.

Hii ni hadithi ya mtu mmoja,hebu natuangalia ya walio wengi.Waswahili wana msemo wao kuwa penye wengi hapaharibiki neno.Kikako cha ***Haiatul kibarul ulaamau*** kilichokaa chini ya uongozi wa skh Abdul Aziz bin Baaz.Hawa waliokaa hapo wala si makhurafi.Mwishoni wanachuoni hawa walisema kila watu wana kuuona kwao mwezi.Habari za kikao hiki zimeandikwa kwenye gazeti la **Ad-da'awa** toleo nambari 713 ukurasa wa 6, la mwezi 29 Ramadhani mwaka 1399 hijriya.

Sasa hebu tuangalie maneno ya ndugu yetu skh Jaabir,aliposema kuitumia hadithi ya Kuraib kuwa ndio dalili sio sahihi.Nadhani tangu tulikotokea mpaka hapa inaonesha kuwa kuitumia hadithi hii ndiko sahihi.

Katika kuyaendea mambo haya lazima tutumie ***nusuus***,tutumie akili na tuangalie jinsi ambavyo tumeachwa na hao tunaotakiwa tuwaingize katika dini.Kuhusu *nusus* tanazo tayari,ni hizi hadithi.Bwana Mtume ﷺ kasema musifunge mpaka muuone mwezi na musifungue mpaka muuone.Kama hivyo ndivyo ina maana kuwa sote uwezo wa kuuona tunao.

Msimamo wa ***ikhtilaaful mattaali'i*** unamfanya kila mmoja awemo kwenye hadithi hii.Kizuizi cha kutokuuona si jambo linaloendelea kila siku.Ikiwa hukuuona leo utauuona kesho au mtondogoo.Kinyume chake ***ittihaadul mattaali'i*** itakufanya siku zote usiuone,jambo ambalo na wewe ni haki yako katika dini. Ni ipi dalili ya kumtoa mtu kuwa yeye hayumo katika wanaokusudiwa na hadithi hii?.

Tukisema mwezi unaenea,maana yake ni kuwa hukmu ya mwezi imeenea.Sasa kwa mfano mwezi tumeuona, na hapa kwetu Tanzania ni magharibi.Tukishauona mwezi tu na Ramadhani imeingia,na ndio maana twaanza kuswali tarawehe.

Tukienda na mawazo haya kuwa mwezi dunia nzima ni mmoja,wale wenzetu ambao kwao ni alasiri tukiwapelekea salamu tuwaambieje?.Tuwaambie jizuieni msile kwa sababu Ramadhani imeingia.Ni Ramadhani gani hiyo ya robo siku?.Tukiwaambia kuleni,si itakuwa wanakula ndani ya Ramadhani?.Ikiwa wajizuie watakuja lipa,watalipa deni gani ambalo halijatimia?.

Kwa hali hiyo matatizo hayatakwisha,na ili kuyaondoa matatizo hayo ni kwa kila watu kuwa na kuuona kwao mwezi.

Haya tuje kwenye dalili nyengine.Wakati wa Mtume swalla Llaahu alayhi was salam maswahaba waliokuwa mbali naye walikuwa wakifunga vipi?.Bila shaka wako waliokuwa wakifunga tofauti kwa vile hakukuwa na simu na mawasiliano mengine mfano wake.Sasa jee ni ipi sunnah?,kwa sababu hii ndiyo hali aliyotuwacha nayo Mtume swalla Llaahu alayhi was sallam na iliendelea hivyo kwa maswahaba,kwa tabiina mpaka yalipogunduliwa mawasiliano ya kisasa.

Kulazimisha kuwa watu wafunge pamoja ni kulazimisha jambo ambalo halikuwepo wakati wa Mtume Mtume swalla Llaahu alayhi was-salam.Hili litapelekea uislamu kuwa na ukarabati mwingi.

Wale wanaosema kuwa Abdullah ibnu Abbas aliukutaa mwezi wa Kuraib kwa kuwa ni mmoja na mmoja hakubaliwi katika kufungua.Mantiki yake ni kuwa lau wangekuwa wengi basi angewakubali.,twende hivyo hivyo kuwa hakuukubali,sasa tupeni ***nass*** ya kuonesha

kuwa Abdullah ibnu Abbas aliilipa siku hiyo au kwamba watu wa Madina waliilipa.Sisi hatulazimishi kuwa walipe kwa sababu kila watu wana kuuona kwao.

Hoja ya kuwa watu watumie mwezi mmoja ni hoja ya watu wenye uwezo,kulazimisha kuwa kila mmoja amiliki simu,au awe na televisheni.Jee uislamu utekelezwe vizuri na watu wenye uwezo tu, na wale wasio na uwezo ndio watekeleze ovyo ovyo ?,ilhali Uislamu ni dini ya usawa.

Namalizia na hoja ya ndugu yangu skh Jaabir kuwa Arafa ikishakupita kule ndio imetoka hiyo !.Wewe unaefunga huku wafunga jambo gani?, na limeshapita!.Sisi twasema lile jambo lipo,bali kule limewahi na hapa limechelewa.Mfano swala ya Alasiri inamalizikia jua linapozama.Mimi niliyeko Dar es salaam kwangu jua limezama nitaswali Magharibi,lakini kwa wenzetu Mwanza jua bado liko,sasa jee nitawazuilia watu wa Mwanza wasiswali Alasiri?.Watakaouliza,jawabu ni kwamba jua limezama Dar es salaam lakini Mwanza jua bado lipo!.

Wassalaam alaykum warahmatuLlaah.

- **HOJA ZA ANSAAR SUNNA**
  SHEIKH SALIM MSABAH

Sheikh Salim Msabah alirudi tena baada ya kuondoka skh Muhammed Iddi,akaanza kw kusema:

Nakubaliana na maneno ya skh Ahmad Zubeir kuwa hakuna uislamu wa kitaifa na wa kimataifa,lakini kwenye uislamu tofauti za rai zinakubalika ndio maana tuko hapa na Qur'an 42:10 inalikubali hili.

Kuhusu fatawa za skh Qardhawiy kuwa waislamu sote tunatakiwa kufuata maamuzi ya mufti au vyombo vyenye mamlaka kama skh Ahmad Zubeir alivyotaka tuamini.Hata hivyo ukiangalia vizuri kitabu hicho cha fatawa za Alqardhawiy jz 2 mwisho wa hoja hiyo, Sheikh Qardhawiy kasema katika nchi ya kiislamu.Lakini nchi yetu ina mazingira tafauti.

Katiba ya Jamhuri ya Muugano wa Tanzania kifungu cha 19 sehemu ya kwanza inasema kila mtu ana uhuru wa kuchagua na kuabudu katika mambo ya kiimani.Kwenye katiba ya Bakwata ibara ya 88 inataja mamlaka ya kamati ya maulamaa.Mamlaka ya 2 imetajwa ya kuwa kamati ina mamlaka ya kutoa maamuzi katika mambo ambayo hukumu yake iko kwenye Qur'an moja kwa moja.

Sheikh Ahmad Zubeir katusaidia aliposema kuwa kwa suala hili tunakubaliana kwenye ***mantuq*** lakini tunatafautiana katika ***mafhum***.Ukiwacha suala la kuuona mwezi,hatusemi kuwa suala hili halimo katika Qur'an,lakini lina tofauti za wazi miongoni mwa wanavyuoni.

Kwenye vitabu vya fiqhi vinavyoeleza mamlaka ya mufti imeelezwa kuwa anayetafuta fatwa ana hiyari ya kuifuata fatwa aliyopewa au kufuata nyengine atakayoiona iko karibu zaidi na dalili za kisheria.Mufti hana mamlaka ya kutumia nguvu kushurutisha fatwa yake ifuatwe.Yeye juu yake ni kumjuvya tu mwenye kuhitaji.

Kwa kipengele hiki twataka kusema kuwa tusilazimishane kufuata kauli ya mufti.Sheikh Ahmad kasema tufuate ***waliul amr***.Lakini kwa maana ya ***waliul amr***,basi ***waliul amr*** wa hapa atakuwa ni raisi wa nchi.Tukisema kuwa pana uhawilishaji wa mamlaka bado pana utata,kwa sababu serikali imesema haina dini.Kwa maana hiyo hapa hatuna ***waliul amr***.Iwapo ni kukaa kumchagua hakuna miongoni mwetu anayekataa .

Suala lililoulizwa kuhusu Arafa iwapo ni ***dharfu makaan*** au ***dharfu zaman***?.Kwa mujibu wa Qur'an 2:198,Arafa ni ***dharfu makaan***.Kisheria ni ***dharfu makaan*** na ***dharfu zaman***,kwa sababu hadithi za Mtume صلى الله عليه و سلم zinazozungumzia kufunga Arafa ni kwa kielelezo cha wakati(zamaan).

Sheikh Muhammed Iddi amesema anatetea hoja za upande wao na sisi tumeambiwa hatujajibu hoja.Kama mumeangalia vyema ratiba mutaona kuwa sisi tulitakiwa kutoa hoja tu na nyinyi kujibu hoja.Badala yake tunarefusha kikao kwa kukaa kujibu hoja mpya.

Sisi hatukatai kuwa iko kuangalia mwezi kwa kutumia matlai,hata kwenye vitabu pia ipo.Lakini musitarajie kuwa tutakaa hapa kutetea msimamo huu,kwa sababu tumeona kuwa ni mtazamo dhaifu na hauna maslahi na uislamu.Miaka yote hiyo tuliukubali,lakini tulipoona ni msimamo wenye mapungufu tumeukataa kutokana na hoja tulizonazo.Suala ni hoja ***raajih*** na ***marjuuh***.

Nyinyi ndio ambao tumezoea kuwaona mukikataa hoja zenye nguvu za msimamo wetu,ya kuwa mwezi ukionekana pahala popote duniani basi waislamu wanapaswa kuufuata, pamoja na kuwa mumekubali kuwa na mtazamo huu pia upo, kama alivyosema skh Ahmad Zubeir.

Kuhusu fatwa ya Ibnu Baaz,sisi tunayo fatwa iliyotoka mwaka 1994 ambayo ina maelezo tofauti na hayo ambayo nyinyi mumeyanakili.Anaonesha kuwa habari hii ya ***ikhtilaaful mattaali'i*** si jambo la kuzingatiwa.

Aliulizwa watu wafungeje wakikhitilafiana ***mattaali'i***?.Jee watu wa miji ya mbali kama Marekani na Australia itawafalia kufunga kwa muono wa watu wa Saudi Arabia?.Akajibu kuwa lililo sahihi ni kutegemea kuonekana kwa mwezi na kuacha kufuata machimbuko ya jua kwa sababu Mtume ﷺ aliamrisha tutegemee kuonekana kwa mwezi na hakufafanua juu ya hilo, na wala hakuashiria juu ya matumizi ya machomozo ya jua ilhali anayajua hayo.

Hayo ni maelezo ya Ibnu Baaz.Ikiwa mtu atataka kujibu basi naajibu.

Kama tulivyosema kabla kuwa hili suala ni **mutlaq**,na **mutlaq ki usulul fiqh** huchukuliwa kwa hali yake lilivyo mpaka kupatikane **itaqid**.Kwa hili Mtume ﷺ hakuwahi kufunga kwa kutumia ***mattaali'i*****,**hivyo na sisi tusifunge kwa kutumia machomozo hayo.

Tunamalizia kwa hoja ya sheikh Muhammed Idd,aliposema kuwa " sisi tunafuata mapokezi ya Kuraib kuwa ndiyo dalili yetu".Sisi hatukatai kuwa mapokezi hayo yapo na yamefuatwa na wanachuoni wengine.Sisi kwa upande wetu tumemuwacha mwanachuoni kwa kufuata mwanachuoni mwengine.Huu ndio utaratibu wa kiislamu.

Hebu natumuangalie imamu Suyuttiy,mwanachuoni wa kishaafiy katika sherh yake ya **Sunanu Nasaaiy**.Anasema mapokezi ya Kuraib inaweza kuwa na maana ya kuwa Ibnu Abbas aliukataa mwezi wa Kuraib kwa vile ni ushahidi wa mtu mmoja ambao haukubaliwi katika kufungua.Pia yawezekana kuwa kila mmoja na mwezi wake.Hii ni *possibility* ya 50-50.

Katika hali ya aina hiyo huwa hapasimami hoja,Si hoja kuwa ina sanad yake katika Sahih Muslim,kwa sababu hadithi inaweza kuwa na sanad sahihi lakini dhahiri yake ikawa haifahamiki.Natoa mfano mmoja ya hadithi ya Mtume صلى الله عليه و سلم ambayo hata skh Qardhawiy kaitaja katika kitabu chake ***Kaifa nahtamilu ma'a sunnati Nnabiy***;kuwa ni sunna ya Mtume ﷺ.Hadithi yenyewe ni ***Al waznu; waznu ahli Makkah wal mikyaalu; mikyaalu ahli Madina***.Kwamba kipimo cha uzito ni kwa kufuata kipimo cha watu wa Makkah na ujazo ni kwa kufuata kipimo cha watu wa Madina.

Suali ni jee hii leo sisi twafuata vipimo vya watu wa Makka na Madina au wafaransa na waiengereza?.Jawabu ni kuwa twafuata vipimo vya wafaransa na waiengereza.Sasa jee twamkhalifu Mtume صلى الله عليه و سلم ?.Kidhahiri utaona twamkhalifu,lakini Laa hasha!.hatumkhalifu Mtume صلى الله عليه و سلم .Mtume صلى الله عليه و سلم kwa mazingira ya wakati ule alitaka kusawazisha tu (balance) baina ya watu wa Makka na Madina ili kusiwe na mizozo baina yao.

Watu wa Makka walikuwa wakulima ambao wakitumia zaidi vipimo vya uzito,lakini watu wa Madina ni wafugaji waliokuwa wamezoea vipimo vya ujazo.Sasa hoja ya kwamba watu walikuwa wakifunga kila mmoja na mwezi wake,hivyo hivyo mpaka kwa maswahaba,haina maana kuwa na sisi tufunge hivyo hivyo.***Mafhuum*** ya hadith huwa yanabadilika kutokana na wakati.

Leo wanachuoni wote wamekubali kuwa inajuzu kuhirimia kwenye ndege,kwa nini iwe hivyo ilhali hakuna hata swahaba mmoja aliyepanda na kuhirimia kwenye ndege?.Hii ni kwa sababu Mtume صلى الله عليه و سلم ni rehma kwa walimwengu wote -Qur'an 21:107.Kadiri uislamu unavyosonga mbele ndivyo unavyozidi kueleweka.

Wanachuoni pia wamekiri kuwa baadhi ya aya maswahaba hawakuweza kuzifasiri,sasa ndio zimefasirika vyema,baada ya kupatikana maendeleo ya kiteknolojia.Uislamu ni dini ya wakati wote;uliopita na ujao.

Kuhusu suala kwamba kama ni kufunga kwa mwezi mmoja mbona tunatafautiana kwa nyakati za swala.Kama alivyosema sheikh Muhammed,swala inakuwa ni moja lakini kuna kuchelewa na kutangulia.Kigoma na Bukoba na ukanda wa magharibi wote nyakati zao za swala ni tofauti na watu walioko upande wa mashariki.Hii ni kwa kiwango cha kitaifa.Katika kiwango cha kimataifa upande wa funga pia tunatafautiana.Ikiwa ni kwa tafauti hiyo ,basi tunatafautiana kwa masaa tu.

Ukisema Bombay wanaswali alfajiri na Makka wanaswali adhuhuri ,itakuwaje?.Hili ni suali rahisi tu.Ni kuwa hawa wametangulia na hawa watafuatia!,ni nani wameanza na nani wafuatie ?. Kwenye Qur'an 3:27 inaonesha tafauti hizi za masaa ni zenye dalili.Muhimu ni kuwa katika kufunga hakuna tofauti ya siku nzima.

Kufikia hapa nisimame ili wenzangu nao wapate nafasi ya kuchangia.***Wasalaam alaykum warahamatullaah.***

- ***HOJA ZA BAKWATA***

  Sharifu HUSSEIN HASHIM ABDULQAADIR AL MUSAWIY

Tunamshukuru Allah subhaanahu wataala kwa kutuwezeshesha kukutana hapa katika juhudi ya kutafuta ***islahi baina nnaasi***.Sulhu baina ya watu ni jambo kubwa sana katika uislamu.

Mwanachuoni mmoja alipelekewa salamu kuwa msikitini kwake kuna watu wapigana ngumi kwa kuwa wengine wasema tarawehe ni rakaa ishirini na wengine wasema ni nane tu.Akaambiwa nenda ukawawahi sheikh !.Akawajibu nendeni mukaufunge msikiti haraka .Akaulizwa haya vipi sheikh wasemaje tukaufunge msikiti!.Akasema

ndio!,tarawehe ni suna tu,lakini umoja ni wajibu.Hatuwezi kuacha wajibu kwa kufuata suna.

Katika nukta nilizotayarisha nitaanza na lile la mbele kabla sijalisahau.Ni kuhusu majumuisho ya ustadh Salim Msabah alipokuwa akijibu hoja alizotoa mufti huku akitoa hoja za kuwaunga mkono wao akina Msabah.Alisema kuwa katika kikao cha **Daarul iftah** wanachuoni wengi waliokutana walikubaliana kuwa **mattaali'i** hayazingatiwi.Ni sheikh mmoja tu aliyepinga,kuwa yazingatiwa.Akauliza itakuwaje tuache kufuata walio wengi na tufuate huyu mmmoja?.

Mufti alisema pia kuwa kikao kingine kilifanyika huko huko Saudia na kauli zao zilikuwa zikiunga mkono **mattaali'i** na ndiyo mapendeleo ya mufti .Kwa maksudi kabisa kwa ufundi wa kisiasa na ili kujenga nguvu hoja za upande wao,hili hakulisema.Huyu bwana mwenzetu ni mwanasiasa yeye.

Kuhusu Ibnu Baaz ningewaomba pande zote tukubaliane tumuwache kwenye ***istidlaali*** zetu ,naona zitatupotosha,kwa sababu upande huo wasema wana fatwa zake anaunga mkono **mattaali'i** na upande huu nao wasema wana **qaraari** zake zinazopinga **mattaali'i**,miaka tafauti.Mimi nami nina nyengine inayounga mkono.Au ndio mtindo wao huu hawa Ansaar ; leo kutoa kauli hii na kesho kauli nyengine,kwa sababu huyu Ibnu Baaz ni sheikh wao Ansaar.

Alipouliza tena juu ya pendekezo lake la kumuwacha Ibnu Baaz, sauti kadhaa ndani ya ukumbi zilisikika zikiunga mkono,halafu akaendelea.

Ndugu yangu sheikh Ahmad Zubeir kasema sheikh Tantawiy kakubali kuwa **mattaali'i** ni ya kuzingatiwa.Ndugu yetu sheikh Jaabir naye kasema sheikh Jadal Haq kasema **mattaali'i** si jambo la kuzingatiwa .Hawa wote ni masheikh wa Azhar.Sheikh Tantawiy ndiye aliyeko huko,wakati huu na mufti wetu hapa.

Hadithi ya Mtume صلى الله عليه و سلم ,***swuumuw liru'yatih wa afttiruu li ru'yatih,***kuwa fungeni kwa kuuona mwezi ,na fungueni kwa kuuona.Si kweli kuwa hawa Ansaar wafunga na kufungua kwa kuonekana mwezi popote duniani.Ukweli ni kuwa hawa wana sehemu yao wanayofuata,ni huko huko Saudia walikopatia digrii zao.Hawana cha mwezi kuonekana China wala Pakistan.Wana mawasiliano gani na ulimwengu mzima!.

Tutakwendaje kwa fatwa za Jadal Haq,kuwa ikifika hija ndio tufuate pamoja miezi mitatu ya tarehe za Hija mpaka Arafa?.

Hapa nina gazeti la huko huko Saudia la mwezi 7 Ramadhani 1410,sawa na tarehe 2 Aprili 1990.Hapa sheikh Muhammad Taaj Abdulrahman athibitisha kuwa kila watu wana kuuona kwao mwezi.Katika mengi aliyoyasema mwisho kasema kama walivyotuambia Ansaar waliposoma ya kwao"**wamekubaliana wanachuoni walio wengi……**"kuwa **mattaali'i** ni yenye kuzingatiwa.

Katika kuichambua hadithi ya Ibnu Abbas na Kuraib asema kuwa ;aliposema Ibnu Abbas "*hivi ndivyo alivyotuamrisha Mtume* صلى الله عليه و سلم**"***;* hii ni hoja kuwa hii hadithi ni ***marfu'u*** na ni hoja kuwa machimbuko ya jua kwa kila mji ni jambo lenye kuzingatiwa.Ile kuhudhuria tu hakutoshi lazima ipatikane yakini nako ni kuonekana mwezi.

Akaendelea kutolea dalili juu ya kuzingatiwa machomozo ya jua kwa kuinakili hadithi ambayo twaisoma sana hapa;Musifunge mpaka uonekane mwezi na musifungue mpaka uonekana mwezi.Halafu kasema swaumu imeambatanishwa na kuonekana kwa mwezi kama swala ilivyofungamanishwa na kupenduka kwa jua.Sheikh Shaarawy katika tafsiri yake ya Qur'an kaenda mpaka kaeleza juu ya swala ya wenzetu ambako mara nyingine inafika hadi miezi sita hawalioni jua,na miezi mingine ni mchana tu.

Huyu Salim Msabah ni mtu mzuri sana katika majadiliano.Yeye kaikubali hadithi ya Kuraib kuwa ipo,kuna ushahidi pia sheikh Salim Barahiyaan wa kwetu Tanga ambaye ni gogo la kiansar naye pia kaikubali hadithi hii kuwa ipo.Lakini wenzao wengi wasema hii si hadithi kabisa.Hawajui hata istilahi za hadithi,wasema hiki ni kisa tu na ijtihad za Ibnu Abbas.Hawamtambui Ibnu Abbas kwenye hadithi hii ambaye ni ***hibrul umma***.

Mwisho kwenye maelezo yake kwenye jarida hili asema kuukataa mwezi Ibnu Abbas si kweli kuwa aliukataa kwa kuwa ni ushahidi wa mtu mmoja kama wasemavyo wapinzani wa hoja hii.Ingekuwa ni hivyo basi angemuandikia Muawiya ili kuthibitisha kuonekana mwezi huko na Muawiya naye angemuandikia Ibnu Abbas kuthibitisha kuonekana mwezi huo.Kwa kukosekana kupatikana hilo ni uthibitisho wa kuwa kila watu wana kuuona kwao kwa mwezi,vile vile ilivyokuwa wakati wa Mtume صلى الله عليه و سلم .

Asema nyongeza juu ya maelezo hayo yaliyotangulia ni kuwa Alghasaaniy na Harbiy wamesema kuwa mabedui wa milima ya Najd walimjulisha Mtume صلى الله عليه و سلم kuwa sisi huwa tunawatangulia watu wa Madina kwa kuuona mwezi kwa siku nzima.Mtume صلى الله عليه و سلم akawajibu kuwa..***Wana watu wa kila mji na kuuona kwao***.Mupo hapo!.

Ngoja sasa niwasomee tamko la Ansaar wa Tanga walilotoa juu ya tamko la makamo wa rais alilolitoa kwenye baraza la Idi tarehe 30.1.1998.Tamko hili limesainiwa na mwenyewe mudiir wa Ansaar-Tanga,sheikh Salim AbdurRahiim.Wasema**:…*Vile vile kisa cha Kuraib alichokitaja mufti wa Bakwata chathibitisha kuwa serikali ya kiislamu iliyokuwa na makao makuu yake Damascus- Shaam (Syria), hawakuwalazimisha waislamu wa Madina kufunga pamoja na watu wa Shaam…***.

Watu wa Shaam nao hawakuwalazimisha waislamu wa Syria kufunga na watu wa Madina,yaani kila watu wakifunga kivyao.Kwa maana hii na Salim AbdurRahiim naye akubali kuwa kila watu wafunge kivyao.Wasichokitaka wao ni kulazimishwa tu,lakini wakitambua kisa cha Kuraib kuwa kipo.

Mpaka hapo **wassalaam alaykum warahmatu llaah**.

- **HOJA ZA ANSAAR SUNNA**
  Sheikh IDRIS OMAR NGALU

Kwanza nataka niwaeleze kuwa kikao hiki, pamoja na ukubwa wake lakini hakifanani na kikako cha mwaka 1970,kilichofanyika Islamic Centre,pale Chng'ombe;Dar es Salaam.

Kikao hicho kilihudhuriwa na masheikh kutoka mikoa yote ya Tanzania na Zanzibar,kama inavyosomeka kwenye jalada la maazimio ya kikao hicho.Baada ya ***Bismillahir Rahmaanir Rahiim***:***BARAZA KUU LA WAISLAMU WA TANZANIA-Mazungumzo na maazimio ya mkutano wa masheikh uliofanyika katika chuo kikuu kikuu cha kiislamu tarehe 19/12/1970.mpaka 22/12/1970,Kikao cha 1.***

Wazee wetu hawa baadhi yao wameshatangulia.Mwenyezi Mungu awarehemu,na wale walio hai awaongoze tuende nao kwa salama. Miongoni mwa mambo ambayo waliyazungumzia ni mada hii ya mwezi.

Sheikh Idris akainua kitabu hicho cha maazimio ambacho sehemu ya juu ilikuwa imenyofolewa na wadudu au kuathirika na maji.Akaonesha picha za masheikh wote waliohudhuria kikao hicho, halafu akasema:

Nataraji kitabu hichi kipo kwenye ofisi zetu za Bakwata na hakuna gogoro kuwa kimezuliwa.

Mufti wetu;sheikh Hemed bin Jumaa bin Hemed ni miongoni mwa waliohudhuria na ana mchango wake katika mazungumzo haya ya kheri.Mzee wetu na mwenyekiti wetu sheikh Issa bin Shaaban bin Simba naye pia alikuwepo.Sasa nawaomba tusikizane yale ambayo masheikh zetu walizungumza mwaka 1970.

Huu ni ukurasa wa 10 ajenda ya 14/70.Umeanza hivi;**Bismillahiir Rahmaanir Rahiim**:**TOFAUTI ZA KUFUNGA NA KUFUNGUA RAMADHANI.**

“ Katika mikoa iliyojibu kuhusu tatizo hili,masheikh wa mikoa hiyo iliyojibu waliafikiana kuwa popote mwezi utakapoonekana katika sehemu yoyote ya Tanzania na ukathibitishwa kwa mujibu wa sheria,yaani kuonekana na mwanamume mmoja ,mtu mzima muadilifu, kuwa ameuona mwezi basi watu waliomo Tanzania watakuwa wana wajibu wa kufunga au kufungua vyovyote itakavyokuwa.”

Masheikh zetu hawa kwanza walikubaliana kwa mujibu wa mipaka ya Tanzania tu. Inaendelea:

“Lakini kulikuwa na baadhi ya masheikh ambao waliona kuwa mwezi ukionekana kwa masafa ya zaidi ya ***qasri***,yaani zaidi ya maili 58 kama vile Tabora na Kigoma basi watu wa Tabora hawawezi kufunga wala kufungua kwa kuonekana mwezi Kigoma.”

Hili ni kundi la pili la masheikh hao,Mwenyezi Mungu awarehemu.Wao tofauti na wenzao wamelifinya eneo na kuwa si zaidi ya meli 58.Kwamba mwezi ukionekana Dar es Salaam huwezi kuwapelekea habari hata waliopo Chalinze.Utaona suala hili sio sisi tu Ahlu Sunna wa leo,hata wazee wetu liliwasumbua vichwa.Inaendelea:

“ Tatizo hili,mkutano uliona kwamba limekuja kwa sababu ya kuelewa vingine aya ya Qur’an tukufu na hadithi za Mtume صلى الله عليه و سلم swalla .Mungu (s.w) amesema mwenye kuushuhudia mwezi miongoni mwa nyinyi naafunge mwezi huo (Ramadhani). Watu hufasiri neno ***shahida*** kwa maana ya kuona,lakini neno hili lina maana mbili.Moja ni hiyo ya kuona na nyengine ni ya kushuhudia.”

“ Kutaka kujua ni maana ipi iliyokusudiwa au iliyopendelewa katika tafsiri hizi mbili,ni kuangalia yale maana iliyopewa.Ikiwa tutachukua maana ya kuona kwanza basi itakuwa Mwenyezi Mungu (s.w) amemlazimisha kufunga yule mwenye macho tu ya kuona.Lakini yule aliye kipofu asiye na macho itakuwa haikumuwajibikia ibada hii ya kufunga.Na hivi ni wazi kuwa sivyo Mwenyezi Mungu (s.w) alivyokusudia.”

“ Vile vile ikiwa ni kuona kwa macho Mwenyezi Mungu ametaja ***shahra*** yenye maana ya mwezi wa siku 29 au 30, na wala si ule mwezi wa kuandama.Kama ni ule mwezi wa kuandama basi Mwenyezi Mungu asingesema namuufunge,kwani mwezi wa kuandama haufungwi bali kifungwacho ni siku.Kwa hivyo ni dhahiri kuwa maana iliyopendelewa ni ile ya kuuhudhuria kwa yoyote yule aliye hai afunge, akiwa na macho au kipofu.Iwe ameuona mwezi kwa macho yake au umethibiti tu kuonekana kwake.”

Nataka ifahamike kuwa gogoro hili halikuletwa na sisi Ansaaru Sunna ,bali limekuwepo tangu 1970 na limeshughulikiwa na wazee wetu hawo,naendelea:

“Ama kuhusu hadithi ya Mtume صلى الله عليه و سلم isemayo fungeni kwa kuonekana mwezi na fungueni kwa kuonekana kwake,hakuwa amewakusudia watu wa Madina tu, bali watu wa ulimwengu mzima,kwamba popote mwezi utakapoonekana basi itawalazimu wafunge.”

Hii ni kauli ya masheikh zetu hao waliokutana mwaka 1970.Vijana wa Ansaaru Sunna wanapofunga kwa kufuata muwafaka wa masheikh zetu wanaonekana ni kioja,lakini kumbe kivitendo wao ndio wanatekeleza kauli za Bakwata.

Tamko hili lilionekana ni la kushtukiza kwa masheikh wa upande wa Bakwata,likawafanya waangaliane baina yao na kushindwa kujizuia,wakawa wakicheka baina yao kwa sauti na kujikausha kuzuia vicheko vyao.

Kwa hivyo sisi msimamo wetu uko pale pale kuwa tutaendelea kufuata mwandamo wa kimataifa kama wazee wetu hawa walivyokubaliana. Tunaendelea:

"Maimamu waliweka kigezo cha mipaka na **masafatul qasr**,kwa sababu kwa siku zao haikuwa rahisi kumtoa mtu Madina na kumpeleka mji mwengine.Kwa mfano kuwaandikia watu wa Tabora kungewachua mwezi mzima habari hizo kuwafikia.Ndipo maimamu wakaweka mpaka huo.Lakini kwa siku za leo zenye maredio na simu na televisheni, habari inaweza kufika popote ulimwenguni kwa robo dakika tu.Mipaka ya namna kama hiyo haiwezi kufanya kazi yake iliyokusudiwa."

Masheikh ambao wanacho kitabu hichi habari hiyo itakuwa wanaijua.Kama Bakwata ina kauli nyengine kinyume na hii basi tuelezwe.

Mmoja ya masheikh upande wa Bakwata akamtaka asome kauli hiyo aliyoiulizia mule mule kwenye kijitabu sheikh Idris alichokuwa akikisoma.Ikasababisha kutoleana ukali kidogo baina yao, hali iliyotulizwa na wajumbe wengine,halafu akaendelea:

Halafu nataka kumzindua kidogo mzee wangu pale.Kuna maneno yaliyotolewa na katibu muhtasi wa mufti kwamba mazungumzo yetu haya ya kheri haturuhusu watu kutoka nje ya Tanzania.Mwengine kasema hawa ni watu wa Saudia.Sasa nataka kumtanabahisha kuwa sisi si wasaudia,sisi ni watanzania!.

Kuhusu hadithi hii ya Kuraib,labda mutufundishe kaida za kilugha.Kwa sababu nikimwambia kaka yangu Athumani Matata;Jee hutoswali swala ya alasiri hapa?.Kuna jawabu za aina mbili.Akijibu ndio!,maana yake nini?.Ataswali hapa au hatoswali?.Kwa kaida za kilugha maana yake ni kuwa hatoswali.Akijibu Hapana!,itakuwa nimemfahamu kaka yangu kuwa anakusudia;kwanini isiwe hivyo?,Nitaswali hapa.

Huyu Kuraib tumemtafiti na kuona ni ***majhuul ain wa swifa***.Alipomwambia Ibnu Abbas **Alaa taktafiy biru'yat Muawiyah wa swiyaamih?**.Jibu lilikuja kwa njia ya ***naf'yi;Laa!.***Kwa vitabu tulivyonavyo, hapo ilikuwa ni *fullstop*.Sasa **naf'yu** ikifuatiwa na jibu la **naf'yu** maana yake ni kuwa Ibnu Abbas kaukubali mwezi aliokuja nao Kuraib.

Mpaka hapa **wassalaam alaykum warahmatuLlaah**.

- **HOJA ZA BAKWATA**

Sheikh ATHUMAN MATATA

Kwanza nasisitiza kwa kuungana mkono na sheikh wetu kutoka Tanga,kuwa si kweli kuwa wao wanafunga kwa kufuata kuonekana mwezi popote ulimwenguni.Imesadifu kuwa kila mara Saudia wakianza kufungua au kufungua basi huwa na wao ndipo wanapofanya hivyo.Hatujawahi kuwasikia leo Pakistan wameuona na sisi twafunga.

Nataka niwaulize wenzetu upande wa Ansaaru Sunnah ,sijui wanafahamu kuwa mwezi kabla ya kuandama huwa unazaliwa ?.Ukitaka usitake lazima saa 20 zipite kabla ya kuandama.Mtume صلى الله عليه و سلم katukataza kujifananisha na mayahudi.Hukumu ya bwana Mtume صلى الله عليه و سلم ni kuwa lazima mwezi uandame,lakini kwa mayahudi ni pale unapozaliwa ndipo wanapoanza mambo yao ya tarehe.

Hapa ninayo kalenda ya ***University of Science –Malaysia***,na gazeti kutoka **North American students Association.**Wote hawa wanailaumu Saudia.

Kwanza nitawasomea tuone nini wamarekani wanachokisema,halafu tuangalie ***International Islamic calendar*** ambayo imesibu kuwa kila sisi tunapofunga imekubali kuwa hivyo ndivyo na tukifungua pia imekubali kuwa hivyo ndivyo.

Sasa sijui Saudia imepatwa na nini,kwa sababu kuna ushahidi kuwa mwaka huu walipofunga hata ilipofika mwezi 30 basi bado mwezi ilikuwa kwao ni shida kuonekana.Mwezi unakuwa na tabu kuonekana mwezi 29,lakini ikifika 30 ya kweli basi lazima uonekane.

Mwezi ukizaliwa saa 2 asubuhi hapa kwetu, baada ya masaa 20 itakuwa ni saa 4 usiku, na mwezi hauwezi kuandama tena wakati huo.Mwezi ni lazima uandame magharibi.Kwa mwezi uliozaliwa saa 2 itabidi uonekane kesho.

Tuone hapa hawa wamarekani walivyotuchorea ***Parabola* za *Conjuction*** wakati mwezi unapozaliwa,yaani wapi utaonekana na wapi hauwezi kuonekana.Imeandikwa:

The visibility criterion has been adjourned by the noble prophet of Allah*, upon whom be peace.The *moon birth criterion is followed by Jews, the practice prohibited by the noble prophet.It is interesting to note that the Saudi regime who claim to be the guardian of the most noble sanctuaries of Islam should insist on following the jewish practice.Their agencies and followers around the world have added to the confusion by insisting on the correctness of the Saudi announcements…….The record of the past 25 years has shown that the Saudis get it wrong each and every time.What they have succeeded in doing though, and through their agencies is, they have succeeded in dividing the ummah.This must be their primary objective,otherwise there is no reason at all for this irrational behaviour.

Wanasema: ***Hukumu ya kuonekana kwa mwezi imeamrishwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani zimshukie,na hukumu ya kuzaliwa kwa mwezi inafuatwa na mayahudi,kitu ambacho Mtume*** صلى الله عليه و سلم ***kakikataza.Inachekesha kuona kuwa Saudia ambao wao wanadai ndio walinzi wa haramu mbili, wanafuata mtindo wa kiyahudi jambo alilolikataza Mtume wa Mwenyezi Mungu.Wafuasi wao ulimwenguni kote wameongeza mgogoro huu kwa kukazania kuwa Tangazo la Saudia ndilo sahihi.***

Sasa rekodi ya miaka 25 iliyopita yaonesha kuwa kila siku na kila wakati wakisema wao hivi ndivyo,inakuwa sivyo na inakuwa wamekosea.Labda walichofanikiwa kukifanya ni kuugawa umma wa kiislamu.

Hivi ndivyo anavyosema huyu mtu wa Amerika.

Baada ya hapo sheikh Athuman akachukua karatasi lenye picha akawaonesha wajumbe parabola ya maeneo mwezi unapoweza kuonekana na maeneo yasiyoweza kuonekana huku akifafanua kuwa:mwezi huo; mjadala ulipofanyika,kwa mujibu wa parabola hizo ilikuwa uonekane tarehe 19. Sehemu nyengine usingeonekana.Tarehe 20 ungeonekana sehemu iliyokuwa haikuuona tarehe 19,na wengine wangeuona tarehe 21.Halafu akaendelea:

Labda wenzetu watatueleza inakuwaje?. Kwa sababu hii ndiyo kalenda ambayo wenzetu kule Malaysia wanaitayarisha na kuifanya isiwe na makosa.Katika tarehe walizotuonesha,ni kuwa Ramadhani ya mwaka huu,hii tuliyoifungua juzi,vile tulivyofunga sisi hapa,ndivyo Ramadhani ilivyokuwa imeanza.Kadhaalika tulivyofungua ndivyo ilivyomaliza.

Sasa sijui mwatwambiaje?,ni kuonekana kwa mwezi kama alivyoamrisha bwana Mtume صلى الله عليه و سلم au ni kuzaliwa kwa mwezi kama wanavyofuata mayahudi?.Kwa hivyo sisi kutokana na sababu hiyo,ndiyo maana hatulazimiki kukufuateni.

Yapo magazeti chungu nzima hapa kutoka huko huko Marekani yanayoilaumu Saudia.*Akaonesha rundo hilo halafu akaendelea*:Lakini kwa kifupi hii ndiyo sayansi inavyosema.Salim Msabah anaposema tunakwenda kisayansi,hii ndiyo sayansi tunaomba atujibu.

Wassalaam alaykum warahmatu Llaah.

- **HOJA ZA ANSAAR SUNNA**
  Sheikh YAHYA HASSAN KHAMIS

Jina langu ni Yahya Hassan Khamis kutoka Arusha.Nachukua nafasi ya sheikh Juma Omar Poli.Napenda kuchangia hoja kutoka tangu pale awali kadri Allah atakavyoniwafiqisha.Kwa vipengele vilivyobaki nitatoa nafasi kwa wenzangu waweze kuendeleza.

Nitaanza kwa hoja ya al akh Ahmad Zubeir pale aliposema kwa kumnukuu skh Muhammad Abdu, kwamba katika Qur'an imesemwa ***Faman shahida minkum falyaswumhu*** na kwa nini isitajwe ***faswuumuuhu….***

Mwenyekiti wa kikako akataka kujua zaidi kuhusu jina lake na nafasi aliyochukua.Sheikh Ahmad Zubeir naye akamrekebisha kuhusu matamshi ya jina la sheikh Muhammad Abdu.Dakika kadhaa zikapita katika marekebisho haya.Hatimae skh Yahya akaonesha kuchoshwa na habari hiyo,kwa ukali akasema "Vipi tena!,mbona twapotezeana muda"*,halafu akaendelea*:

Neno ***man*** katika lugha ya kiarabu kwanza inafanya kazi ya ***ismul mawsul***.Inafaa kutumiwa kwa ***mufrad*** na ***mufradaat***,kwa ***jam'u*** na ***muthanna***.Kwa hivyo katika aya ya Qur'an hapo inaweza kuwa ni ***aam***.Mfano mwengine ni pale Mwenyezi Mungu aliposema katika Qur'an 5:47.Aya imeanza na ***man*** lakini mwisho imemalizia na ***ulaaika*** yenye maana ya ambao(wengi),badala ya ***dhaalika*** ambayo ndiyo ingekuwa na maana ambaye(mmoja).

Sheikh Muhammed Iddi akinukuu kitabu cha **Faidhul ilaah Maalik**,amesema mwenye kitabu kasema si lazima kwa watu kufunga kwa kufuata mwezi wa watu wengine.Napenda kulizungumzia suala hili kwa sura kwamba Mtume صلى الله عليه و سلم akizungumza na umma anazungumza kwa daraja lake kuwa yeye ni kiongozi wa ulimwengu mzima,hivyo huwa anazungumza na umma wake wote popote pale ulipo

Kwa hivyo anapozungumza jambo ambalo ni ***muttlaqa,***hivyo itachukuliwa kuwa ni hivyo hivyo mpaka itakapopatikana dalili iliyo wazi kuwa aliwakusudia watu maalum.

Neno ***ruiya*** katika lugha ya kiarabu hutumika kwa maana tatu,***ru'iya baswaria,ru'iya ilmiya*** **na** ***ru'iya manamiya***.Hizi ***ru'iya*** mbili za mwanzo;***baswariya*** na ***ilmiya*** ndizo alizozikusudia Mtume swalla Llaahu alayhi wa sallam pale aliposema ***swuumuu li ru'yatih wa afttiruu liru'yatih.***Yaani alikusudia ***swuumuu idhaa abswartumuuhu wa afttiruu idhaa abswartumuuh***.Kwa maana nyengine ***swuumuu idhaa sami'itum annaa ikhwaanakum abswaruuh***

Kwa kuzingatia mantiki ya maana hizo ndio maana maimamu wote wanne wamekubaliana kuwa kuona kwa muislamu mmoja huwa ni kuona kwa waislamu wote,madam habari za uoni huo zitawafikia waislamu wengine kwa njia zilizo thabiti.

Sheikh Muhammad Ally Swaabuny katika tafsiri yake ya **Rawaaihul Bayaan** jz1,kasema,wamekubaliana maimamu wanne;Shaafiy,Hanafi,Malik na Hambali kuwa hakuna mazingatio katika kutafautiana miandamo ya mwezi.Bali wakiuona watu wa mji fulani au nchi fulani,basi kuona kwao hao ndio kuona kwa wale wengine.Hivyo ni kwa sababu Mtume صلى الله عليه و سلم alikuwa akizungumza jambo,alikuwa akizungumza na wale waliokuwa mbele yake na wale walioko mbali naye na wa zama zote watakaokuja.

Imamu Alqurttubiy katika kitabu chake **Jaamiul Ahkaamil Qur'an**,kwenye jz 2 ukurasa wa 295 kasema;***idhaa thabata anna ahla baladin ra'auh*** ……Ikiwa watu wa mji fulani wameuona mwezi na wakafunga,na watu wa mji mwengine hawakuuona mwezi na wakawa hawakufunga hali ya kuwa walipata habari za wale waliouona ni juu yao hawa kulipa kadhaa kwa wale waliouna.Kauli hii ndiyo iliyozungumzwa na Laith na wenzake.

Mwenyezi Mungu (s.w) katika Qur'an;suratu Yaasin(36),aya ya 39 isemayo:***Na mwezi tumeupimia vituo mpaka unakuwa kama karara kongwe.***Miongoni mwa walioifasiri aya hii ni huyu sheikh Muhammad Alansaary Alqurtubiy. Alipofasir neno ***manaazil*** katika aya hii kasema vituo vilivyokusudiwa katika Qur'an viko vituo 28.Mwezi huwa katika kituo kimoja kila usiku na ukipita usiku huo mwezi huhama kituo hicho na kuhamia katika kituo kingine.

Vituo hivyo akavitaja kuwa ni 1.AlShurttaan,2.AlBattiin,3.AlThariya 4.Aldabiraan 5.Alhafiat 6.Al aniat 7.Aldhiraau 8.Al nathrat 9.Alttaraf 10.Alkharataan 11.Alsarfa 12.Al awaau 13.Alsamak 14.Alghafir 15.Azzabaaniyaan 16.Al iklliil 17.Alqalbu 18.Al shuulat 19.Alnaaim 20. Albulda 21.Saad aldhaabih 22.Saad balagh 23.Saad alsuud 24.Saad 25. Al akhbiyat 26.Al faragh almuqdam 27.Al faragh al aakhir 28.Buttun al huutt.

Kisha akasema mwezi ukifika kituo cha mwisho hurudia cha mwanzo kuanza mzunguuko mpya .Anasema muhimili wa mzunguko wa mwezi hupitia kwenye vituo hivyo 28 kwa siku 28.Baada ya hapo huonekana ukiwa ni mwezi mchanga.

Sasa nasema kuwa Mwenyezi Mungu (s.w) katika Qur'an anazungumza na binadamu wanaokaa kwenye sayari yenye mwezi mmoja,kwa sababu ziko sayari zina miezi zaidi ya mmoja.Ilivyokuwa yuwazungumza na viumbe hawa wanaokaa kwenye sayari yenye mwezi mmoja, ndipo akasema ***walqamara*** kwamba watu wa mashariki ya mbali au mashariki ya kati, wote wanatumia mwezi huu mmoja.

Kwa hivyo haiwezekani kwa watu hawa kuwa na tarehe mbili tafauti,hawa mwezi mosi na hawa mwezi thalathini.Mwenyezi Mungu (s.w) hakusema ***walqamarain*** **au** ***wal aqmara*** kwamba kuna miezi miwili au miezi zaidi ya miwili.

Kuna hadithi Mtume صلى الله عليه و سلم anayosema kuwa Ramadhani ikianza milango ya motoni hufungwa na milango ya pepo hufunguliwa na mashetani nao hufungwa.Sasa kuna dalili gani kuwa Ramadhani inapoanza milango ya kule huwa imefungwa na kufunguliwa na mashetani kutiwa pingu,lakini kwetu Tanzania huwa bado?.Jee hii mipaka ya kijiografia iliyowekwa na wakoloni kwa Mungu nako katika kujenga pepo na moto na kufungwa mashetani nayo ni ***mu'utabara*** au ni ***ghair mu'utabara***?.

Kuna rai imetolewa hapa kuwa tumuwache sheikh Abdul Aziz bin Baaz katika kufuata fatwa zake kwa sababu ana kauli zinazokosana.Jambo hili katika uislamu ni ***jaiz*** *na* ipo mifano mingi sana katika uislamu,kwa sababu msafara wa kutafuta elimu ni mrefu kabisa.Hakuna hata mmoja ambaye ataufikia kileleni.Kila siku atapata jambo jipya analoweza kuona hili ni bora kuliko kule ninakotoka,hivyo akaliwacha lile na kufuata lililobora.

Katika fiqhi ya imamu Shaafiy tumeona kuna ***Qaulun jadiid*** na ***qaulun qadiim***,hii ni kwa sababu katika maisha yake yote yeye alikuwa daima anasoma na alikuwa anaona vitu vipya..Anasemaje imamu Shaafiy?;***ayyu s- samaai tudhwiluniy wa ayyul ardh tuqiluniy idhaa rawaitu min rasuuli Llaah walam aqul alal ainiy wal raas.Mahmaa qultu min qauliy wa mahmaa ahadtu min markhadiy wa fiyhi anir rasuuli lIaah khilaafu maa qultu, fal qaulu maa qaala rasuulu Llaah wa huwa qauliy.***

Ni mbingu ya nani itakayonifunika na ardhi ya nani itakayonibeba, pindi mimi nitakapoletewa habari kutoka kwa Mtume swalla llaahu alayhi wa sallam zilizothibiti, kisha mimi nisizipokee habari hizo kwa macho na akili yangu yote.Popote nitakaposema chochote kwa ijtihadi yangu na popote nitakapochukua chochote na kutoka katika kauli hiyo ikawa kuna maneno yangu yanayotofautiana na kauli muliyoipata nyinyi kutoka kwa Mtume صلى الله عليه و سلم.Basi maneno na msimamo wangu basi ni yale yaliyosemwa na Mtume صلى الله عليه و سلم . Na hiyo ndiyo kauli yangu

Yaani imamu Shaafiy yuko radhi kuachwa kauli yake,hivyo na sheikh Ibnu Baaz juzi kusema kauli nyengine na leo kusema kauli nyengine ni mambo ambayo yanakubalika katika uislamu.

Tuje kwenye habari kuwa sisi tunafuata mwezi wa kuzaliwa na si mwezi wa kuandama.Hizi ni habari ambazo si za kweli.Mimi nilikuwa nina kalenda ambayo niliinunua mjini Makka,ya mwaka huu ambao tumeumaliza.Nitainasibisha na Saudi Arabia.Mwezi Shaaban kwa mujibu wa kalenda ile niliyoinunua ulikuwa na siku 30,lakini Shaaban waliyoitangaza kuwa mwezi umeandama ulikuwa na siku 29 tu.Ushahidi mwengine ni kuwa kabla mwezi kwisha huwa wanatangaza kuwa yoyote atakayeuona mwezi alete habari na nambari za simu hutolewa.Hivyo si kweli kuwa sisi tunakwenda na kalenda iliyokwisha kupangwa tangu zamani.Bali mambo ya kalenda yapo na hutumiwa kwa ajili ya masuala ya ***muamalaat*** tu.

Tumeambiwa habari ya watu ambao kwao hawakuuona mwezi kwa muda wa miezi 6.Hapa ninaye ustadh alipokuwa akizungumza kuhusu watu hao kuonesha kuwa Mtume صلى الله عليه و سلم alikuwa ni kiongozi kwa watu wa ulimwengu mzima.Anasema wale ambao hawauoni mwezi kama wale wanaokaa maeneo ya ncha ya kaskazini; ***khuttuutu shimaali***,hawa ni juu yao wakadirie,na makadirio yao hayo watayafanya na miji au nchi ambazo masaa ya usiku na mchana yanakaribiana kuwa sawa.Mwisho akaitaja miji hiyo kuwa ni kama Makka na Madina.

Kufikia hapo inshaAllah itakuwa nimeweza kuyaeleza yale niliyokusudia ingawa kwa ufupi.

Wassallaam alaykum warahmatuLlaah.

- **HOJA ZA BAKWATA**

Sheikh AHMAD ZUBEIR

Sheikh Ahmad Zubeir akainua mkono na akachaguliwa kurudi kuchangia kwa mara nyengine.Akarudia kusema kwamba pamoja na yote yaliyozungumzwa hakuna aliyeweza kumuondoa kwenye kiti,na sasa ndiyo kabisa!.Halafu akaendelea:

Nitaanza na ndugu yangu Yahya.Sitaki nimuingilie katika habari zake za ***nahwu*** na ***swarfa***.Kataja ***manaazil***,yahitaji mtu amueleweshe zaidi.Sasa kitu kilichopo ni kuwa, mwezi ni mmoja,hapa hakuna aliye na ukinzani.

Nimesema kuwa sikujua kuwa mjadala utafikia huku,kwa hivyo natumia bongo langu tu.Mtu akisoma **Sunanu Daarul quttni**,jz ya 1 kuhusu habari ya mwezi.Swahaba mmoja alimwendea Mtume صلى الله عليه و سلم akasema tumeuona mwezi,mbaye atauona mdogo atasema tumeuona jana,na atakayesema ni mkubwa atasema ni wa juzi.Kwa maana kuwa sisi tumechelewa kufunga.Mtume صلى الله عليه و سلم akamjibu yule swahaba ***Inna Llaaha ammadahu ilaa ru'uya***.Mwenyezi Mungu سبحانه وتعالى ameupa muda mpaka kuonekanwa.

Yeye ustadh Yahya kakubali pale katika ***maraaji'i*** aliyosoma;***Qadhaa alaa nafsih.***Kasema nchi za mbali zitachukua hukumu kutoka nchi zinazowafikiana…..***Walilaahil hamdu***,tumemaliza hapo.

Sasa kuna jambo jengine,kama alivyosema mdogo wangu na mpenzi wangu wa siku nyingi,Salilm Msabah,mwalimu wetu ni Bakathir. Yaonesha kuwa yeye kakubali tayari lakini tatizo ni kuwa hatuna ***waliul amr*** , kwa sababu nchi yetu si ya kiislamu.Sasa nchi ya kiislamu iweje?,kwa sababu katika nchi kama hizo za Saudia,Kuwait na nyenginezo.Hizi ni nchi za kifalme,jee uislamu unautaka ufalme?.

Kwa hivyo kitu kilichopo ni kama alivyosema sheikh Attiya bin Salim bin Muhammad,na yeye yuko hai Madina anyetaka na aende akamuulize.Anasema:Wale watakaochukua habari ya mwezi nchi nyengine ni ***aqaliatul muslima***,ni waislamu wadogo ambao hawajitambui.Hiyo ni kanda yake ya mwaka huu.

Lakini ukiwachukulia walio wengi,kama sisi hapa Tanzania, tumemchagua mwenzetu kwa hiyari yetu,wee bwana wee !..Kwa sababu ukiangalia mfumo wa Bakwata umeanza tangu shinani.Hakuna katika kila kijiji isipokuwa Bakwata ipo.Sasa wote itakuwa wamemchagua.Kwa hivyo wote hao itakuwa wamemkubali huyu kuwa ni ***waliul amr*** wao.Soma tena kwa Qardhawiy utaona kuthibiti kwa ***waliul amr***.Akitothibitika huyu kuwa ni ***waliul amr*** basi katika ulimwengu wetu wa sasa itakuwa hakuna tena ***waliul amr.***

Ukiangalia serikali zote zina matatizo,ukienda Saudia ,ukienda Misri ni hivyo na kote huko,labda tukienda Bangladesh ambako kuna waislamu wengi zaidi. Hii ni kwa sababu ***waliul amr*** ni mtu ambaye tumemchagua sisi wenyewe ili atuendeshee mambo yetu.Ndivyo alivyotafsiri duktur Muhammad Mustafa alipokuwa akitafsiri aya ya ***waliul amr.***

Waliul amr wetu,mufti wetu akihukumu jambo,ni vile vile kwa ulimwengu mzima hata ukienda Masri na kwengine.Sasa haiwezekani kwa watu wa kundi moja kama hivi sisi,halafu wa kundi jengine wadai jambo jengine,halafu ukasema kuwa tumenyan'ganywa uhuru wa kuabudu,hilo si kweli.Madam sote tumejikubali kuwa ni ***Ansaaru Sunna*** na ni ***Ansaaru Llaah***,sote tunasoma **Sahih Bukhar** na **Sahih Muslim** au vitabu vya imamu Nawawiy.

Haiwezekani kuwa tukubaliane jambo halafu wengine waliharibu kwa ila ya uhuru wa kuabudu.Namalizia kwa kusema kuwa sisi ***waliul amr*** wetu yupo pale pale.Tujibiwe kuwa ni nani ambaye angesema.Jee mtu yoyote tu anaweza kusema?.La mwisho kabisa ni kuhusu Arafa.Kuhusu arafa bwana!,mpaka sasa haijajibika.

Mtume صلى الله عليه و سلم kasema katika **Sahih Muslim** kuwa Malaika wa usiku na mchana huwa wanakutanika wakati wa alfajiri.Kwa maneno mengine huwa wanapeana noba.Sasa jee ni alfajiri ya wapi?.Kwa sababu wanaposwali alfajiri watu wa Makka huku huwa bado hawajaswali,au wengine wamelala au wengine kwao ni mchana!.Suali ni jee,alfajiri ya wapi?..

Mwisho ni ***Innaa anzalnaahu***……Sote tunakubaliana kuwa kuna ***Lailatul qadri***,kweli si kweli,ni kweli!.Na sote tunakubaliana kuwa ***lailatul qadri*** hupatikana alfajiri.Sasa masaa yale yatakuwa ni masaa ya pahala gani?. ?. Kwa sababu tutaifanya elimu ya Mwenyezi Mungu ni ***dhayiq*** si ***waasi'in*** na hii ni sifa ya ***khaain***

Kwa kutoa maelezo hayo kwa njia ya masuali skh Ahmad akamaliza na kukaa.
Baada ya kukaa skh Ahmad mjadala baina ya pande mbili juu ya namna ya kuendesha kikao ukaibuka tena.Dakika kadhaa zikapita kwa kukumbushana makubaliano ya awali.Mmoja kutoka Bakwata akaonesha na kusoma ratiba inavyosema ambapo tukio la mwisho lilikuwa ni hoja kutoka Bakwata.Upande wa Ansaar ukakumbusha kuwa sasa ilikuwa ni zamu yao ya uenyekiti kwa vile ratiba ilijadiliwa kabla.Skh Yussuf Rajab Mlenge upande wa Ansaar sunna akapata nafasi ya kufafanua zaidi kwa kusema.

- **HOJA ZA ANSAAR SUNNA**
  SKH.YUSSUF MNENGE

Mzozo huu wa mwezi upo kwa zaidi ya miaka 20,hivyo kufikiri mjadala wake utamalizika kwa siku moja tu si kweli.Hoja zote tulizozitoa bado hazijajibiwa.Sasa hivi itakuja ***faatiha!***,sasa tutakondoka na uamuzi upi?.

Wakati skh Yussuf akiendelea kueleza na kurusha lawama kwa baadhi ya wazungumzaji upande wa Bakwata,skh Jaabir Katura akainuka na kwenda kuchukua nafasi ya uenyekiti badala ya skh Issa,ambayo ndiyo yaliyokuwa makubaliano ya awali.
Baada ya kukalia kiti cha uenyekiti,skh Jaabir akakumbusha kuwa kwa vile aliyemaliza kuchangia alikuwa kutoka upande wa Bakwata, ambaye angefuata angetoka upande wa Ansaar sunna.
Hata hivyo kabla ya kusimama mchangiaji kutoka Ansaar, akasimama mjumbe kutoka upande wa Bakwata aliyejitambulisha kwa jina la Alhadi bin Musa na kutoa maelezo zaidi kwa kusema.

- **HOJA ZA BAKWATA**
  SKH ALHADI MUSSA

Kwa kuzingatia hoja zilizotolewa na kwa ajili ya kuchunga muda,na kutokana na makubaliano tuliyokubaliana juu ya kuendesha kikao,mimi naona tutapoteza muda mwingi sana na hatutaweza kufikia pahala tulipokusudia,hasa ikiwa tutakwenda na utaratibu huu tunaokwenda nao sasa, kuwa huyu anasema halafu anakuja na huyu anasema.
Tukizingatia kuwa masuala yenyewe yanafahamika;ni ***mas alat ikhtilafia***.Kila mmoja ana dalili za kutosha.Kufikia muafaka si jambo rahisi,hilo sio siri kabisa.Sasa ikiwa kila mmoja atapatiwa nafasi za kujitanua kwa vile anavyotaka hatutofika mwisho. Kwa sababu hoja ni zile zile na zinafanana

Napendekeza hizi hoja zilizotolewa zitoshe na tuingie kipindi cha maasuali na majibu kisha tupeleke kwa wazee wa baraza ili watoe tamko na rai yao ili iweze kujibiwa na upande mwengine.

Mwenyekiti,sheikh Jaabir akaomba maoni kutokana na rai ya skh Alhad.Akauliza:Munaonaje?.Mjumbe kutoka Ansaar akasema kwa vile tumejitolea kwa hili kwa ajili ya Allah (s.w) ni vyema tukubali kupata uzito zaidi ili hili suala tulifikishe mwisho.Ni afadhali tuseme tuliwache kiporo kuliko kuhofia muda.

Mjumbe kutoka Bakwata akasema kwa kweli anaona hoja zilizotolewa zinatosha.Kwa sababu ikiwa ni kujibu haitakuwa rahisi kujibu hoja zote zile zilizoandikwa kwenye karatasi zifikazo 6.Vinginevyo ni kujibebesha mzigo bila sababu.

Akaendelea kutoa hoja mjumbe kutoka Ansaar kwa kupendekeza zitolewe dakika sawa kwa kila upande na uendelezwe utaratibu ulioanzwa tangu mwanzo,isipokuwa pawe na lengo la muda wa mwisho,ijulikane ni saa ngapi.Ikiwa ni dakika tano tano hivyo hivyo mpaka mwisho.Hakuna cha kuchelea kwa sababu hapa hapana ushindani wa Simba na Yanga.

Sharifu Hussein Hashim akapendekeza kuwa kuwe na wazungumzaji wawili wawili kila upande kwa muda wowote watakaopata,si lazima iwe dakika 30 kama wale waliobahatika wa mwanzo.Baada ya hapo iwe ndio mwisho.Rai hii ikakubalika.Mwenyekiti akachagua wa mwanzo kutoka Ansaar Sunna.

Kabla kumsikiliza mzungumzaji huyo. Kwa mara ya pili tunamnakili sharifu Mohammed Sharif Yahya Albaary, kutokana na kipeperushi alichokitoa 3.10.2008,mara baada ya Ramadhani 1429 H,ambayo kama ilivyoanza, ilimalizika katika hali ya kimzozo wa mwezi.Yeye hakuwepo kwenye mjadala wa Kibaha mwaka 1998,kwa kuheshimu mchango wake imebidi kumnakili hapa.Aliandika kama ifuatavyo:

- **HOJA ZA BAKWATA**

SHARIFU MOHAMMED YAHYA

EID MUBARAK

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu, alietuwafikisha kukamilisha mwezi mtukufu wa Ramadhani,kwa kuufunga na tunamuomba atukubalie ibada zetu zote za ndani ya mwezi huo na nyingine.
Haipatikani "EID" bila ya kumalizika kwa mwezi wa Ramadhani.

TUJIKUMBUSHE
Ramadhani ilianza vipi?
Ilianza kwa makundi matatu

A.	Jumapili	Aug	31	2008
B.	Jumatatu	Sept	1	2008
C.	Jumanne	Sept	2	2008

IMEMALIZIKA VIPI?

Imemalizika kwa makundi manne

A.	Jumatatu	Sept	29	2008 (Bila mwezi)
B.	Jumanne	Sept	30	2008 (bila mwezi)
C.	Jumatano	Oct	1	2008 (mwezi/kukamilisha)
D.	Alhamisi	Oct	2	2008 (kukamilisha)

Na hivi ndivyo dunia ilivyoswali EID UL FITR
Jee! Kuna Ramadhani moja na Idd moja Duniani?

MAKUNDI HAYO NI YAPI?

A. Nigeria peke yao safari hii – bila mwezi
B. Nchi zinazofuata Saudi Arabia – bila mwezi ukiondoa Burkina-Faso na Chile (wanaodai kuuona mwezi) na Libya kivyaovyao.
C. Tukiwamo Tanzania ni wa kuuona mwezi na kukamilisha thelathini. Wakiwemo pia Algeria, Australia, Canada, Egypt, Indonesia, Malaysia Oman, Pakistan, Iran, Kenya na nyinginezo nyingi. Kumbuka katika kundi hili kuna chungu nzima zilizoanza na Saudia kufunga lakini hawakufungua nao.
D. Bangladeshi, Barbhados, Germany na India (kukamilisha 30).

TUNAJIFUNZA NINI?

Kila watu wanafunga kivyao,hakuna Ramadhani moja wala Idd moja, na huo ndio umoja wenyewe, ila kwa anaetaka kuuvunja kwa maslahi yake, tena kwa kufunga na kufungua bila kuonekana mwezi.

MWISHO

Tunamshukuru Allah. (S.W) kwa kutuwafikisha kufunga na kufungua kama alivyoelekeza Mtume(S.A.W): kukamilisha Shaabani 30 kwa vile hatukuoona mwezi na kufungua kwa kuona mwezi, Alhamdulillah.

Mohammed Sharif Yahya Albaary
TANGA
3 Shawwal 1429H; 3 October 2008 .

<u>EIDUL ADH-HAA-1429 H</u>

Katika jambo la kufurahisha na kuleta matumaini mema ni kuwa kwa mara ya mwanzo katika kipindi kirefu siku kuu ya mwaka huu hakukuwa na kutofautiana kati ya makundi ya Bakwata na ya Answaaru sunna.

Siku hiyo Disemba 8,2008 ilikuwa ni siku ya furaha kweli kwa waislamu wa Tanzania.Dalili ya umoja wenye kuhitajika sana katika kipindi hiki kigumu ilionekana siku hiyo kwa waislamu wengi kujitokeza kuswali uwanjani.

- **HOJA ZA ANSAAR SUNNA**
  Sheikh HAMZA

Jina langu ni Hamza,ni mtanzania na natokea Dar es Salaam

Kwanza natoa wito tuwache kukosoana kilugha.Kwa sababu hata yule aliyesahihisha jina la Al aamidy kwa tulivyomnakili na yeye pia kakosea.Usahihi wake ni Al ghaamidy.

Haiwezekani kibinadamu kuzungumza kwa muda wa masaa mawili au hata nusu saa na mtu asiponyokwe na neno hata kidogo.Kukosoana itakuwa kama kwamba tumekuja kutoa darsa la kilugha,na hilo sio lengo.

Ama jambo la pili ni kuwa sheikh Ahmad ndiye ambaye ***qadhwaa bi nafsih***.Kwa sababu alipokuja kuzungumza alisema kuwa ibada ya Hija ni ***muta aliq bil qamar***.,na ibada ya swaumu pia ni ***muta aliqu bil qamar illa bi swallaa*** ni ***muta aliqatu bil shams.***Nataraji sijakosea kitu katika kumnukuu.

Sasa ikiwa ni hivyo,swaumu ni sawa, ni ***mutaaliqu bi qamar***,haya hija nayo mwezi wake ni upi?.Ni lazima utakuwa ni ule ule mmoja kama wa kwenye swaumu.Kwa sababu katika hija haiwezekani kila mtu awe na hija yake.Hija ni moja ile ile kwa kila mtu.

Pili nilitaka nizungumzie jambo ambalo limekuwa likirudiwa,kwamba mimi nimezungumza hivi..na imekuwa hivi…..Hapa ni kama kwamba kuna picha inata kujengwa.Kwa mfano hapa tulipokuja kila mtu kakalia kiti alichopewa.Sasa mtu hawezi tena kusema mimi nimekalia kiti hakuna anayeweza kunibandua.Sidhani kuwa kila mmoja ataendelea kubakia hapa ili akalie kiti chake.Kila jambo lina jambo nyuma yake,lakini hili halina.Ninachotaka kusema hapa ni kuwa kiti kimeshaondoka.

Kwa sababu ikiwa ni kuondosha ***khilafia***,ni nani ambaye atachukua jukumu hilo,nafikiri hilo ndilo lililokuwa suala lako.Sasa hili suala lilikuwa tayari linajulikana katika ulimwengu wa kiislamu,hata kabla hao akina Muhammad Abdu hawajaja duniani.Katika Qur'an imeshasemwa katika suratin Nisaa aya ya 59:***Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu,na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi.Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyeezi Mungu na Mtume ,ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.Hayo ndiyo bora zaidi na ndiyo yenye mwisho mwema.***

Katika aya hii Mwenyezi Mungu katupangia mambo matatu,kwanza ni kumtii Yeye Allah سبحانه وتعالى ,kumtii Mtume صلى الله عليه و سلم na kuwatii wenye mamlaka.Lakini pamoja na mpango huo,bado huwa kunazuka ***khilafia*** kama hizi.Sasa inapokuja wapi pa kuitafuta haki,Mwenyezi Mungu kaashiria kwa hao aliowaita waumini,kuwa itafutwe kwenye kitabu chake, na kwenye suna za Mtume صلى الله عليه و سلم.Kaweka na masharti,ya kuwa ikiwa munamuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.Hapo hakuna geni.Kama itakuwa hatuamini hayo basi tutashindwa kuitafuta haki.

Ama kuhusu masuala ya fatwa na kumuweka mufti ,haya mambo yako wazi kabisa.Haya ni masuala ya kisheria,na sheria katika vitabu vyote imeeleza kuwa mufti hana mamlaka

ya kulazimisha jambo,isipokuwa anatoa rai tu.Watu wakitaka watafuata au kutofuata.Ikiwa sheikh una kitabu kinachoeleza kuwa mufti ana jukumu zaidi ya hilo naomba utuletee.

Ama kusema kuwa ndugu yangu Msabah kakubali….hili suala sio kwamba kaleta Msabah.Risala yetu ilikwishaelezea wazi kuwa sisi tunaelewa kuwa suala hili lina khilafu baina ya pande mbili.Kuna wale wanaoona kuwa kila watu na mwezi wao,hao wana dalili zao ambazo tumezieleza.Wako na wale wanaoona kuwa mwandamo ni mmoja tu kwa ulimwengu mzima,hawa wana dalili zao nazo tumezieleza.Sisi kwa upande wetu tumeitakidi na kuziamini dalili za kundi hili.Tangu tunakuja tunalijua hili na ndio maana tumekuja na vitabu vyenye rai zote hizi.

Wewe umekhitari na rai uliyoiona,na sisi tumekhitari na rai zetu.Ndio maana tukasema hapa linalotakiwa ni kusameheana mpaka hapo nyinyi mutakapo***intakili*** mukaja huku tuliko au nyinyi mubaki hapo mulipo na sisi tubaki tulipo.Kwa sababu elimu ni kubadilika kutoka sehemu moja kwenda nyengine.Mimi nimeshangaa sana pale sheikh aliposema kuwa tumuwache Ibnu Baaz kwa vile ana kauli zinazogongana.

Ndugu yangu hapa katoa maelezo yaliyonigusa kuwa hata imamu Shaafiy .Hata elimu yake ya Baghdad ilibadilika alipokuwa akisoma Misri. Sasa huwezi kusema kuwa tuwache madhehebi ya imamu Shaafiy kwa kuwa ali***intakili*** huku na huku.Itakuwa si suala la kielimu.Mwanadamu anapopata elimu hugeuka,na lazima ugeuke.Ndio maana hata Qur'an 98:4 inasema;***Wala hawakufarikiana waliopewa kitabu ila baada ya kuwajia hiyo bayana…***

Ikija elimu lazima ikhitilafu ipo,wapo watakaobadili msimamo wao na wapo watakaobaki na msimamo wao.Kwa kumalizia nasema kuwa kwa msimamo huu tuliokuja nao kila mmoja kati yetu hakuna mwenye neno la kwake alilokuja nalo.Kila mmoja ananakili kutoka katika vitabu au kauli zilizotangulia.Kwa mfano sheikh Yahya alipomnakili skh Ahmad,mwenyekiti aliyeondoka alisema kuwa kauli ile ilikuwa ya skh Muhammad Abdu.Hii ni kuonesha kuwa sote tunanakili tu rai za waliotutangulia.Ama itakuwa unatetea rai za wale wanaosema kila watu na mwezi wao au za wengine wenye msimamo tofauti na huo.

Hapa hakuna kukalia kiti,kila mmoja anaonesha ni namna gani tu alivyofahamu.Ikiwa kila mmoja anajiona kafahamu sahihi cha kufanya ni kuelekezana tu, kila mmoja amkinaishe mwenzake kwa hoja,ili wewe unifuate mimi au mimi nikufuate wewe.Tukifikia pahala tukakubaliana itakuwa tumekuwa wamoja ,na ikiwa si hivyo basi kila mmoja atakuwa ameheshimu utaratibu wa mwenzake.

Kama tukitaka tufikirie zaidi,ni kwamba hili tatizo tunalolizungumza limeanza baada ya miaka 30 tangu kufa kwa Mtume صلى الله عليه و سلم .Hapo ndipo ***ikhtilaaful mattaali'i*** ilipoanza.Hii inahusiana na tukio la Kuraib,hili halikutokea mpaka pale Muawiya alipokuwa mtawala wa Dimashiq au Shaam.

Wakati huo Mtume صلى الله عليه و سلم alikwishakufa,Abubakar (r.a) katawala akafa,sayyidna Omar,Othman (r.a) na Ally (r.a) wote walikwishatawala na kufa.Hapo ndipo Muawiya alipohamisha makao makuu ya serikali ya kiislamu kutoka Madina kwenda Shaam.Tukipenda tunaweza kufanya utafiti,ilikuwaje kabla ya Muawiya,yaani kulikuwa kukifungwaje?.

- **HOJA ZA BAKWATA**
  Skh. MUHANA ABDI

Jina langu naitwa Muhana Abdi.Kabla sijazungumza niliyonayo napenda naeleze mawili matatu.

Sheikh mmoja hapa alisema kuwa wao hawatambui wala hawakubali kupewa hukumu na mufti wa Tanzania.Watu wa kwetu wasema *mwana mkanye akawiya*, yaani mwana ukimkanya mngoje arudi alikokwenda.Kwa sababu ukimkanya wakati keshaparurwa na makucha au keshapigwa vibao ndipo atakapokuelewa.

Wenzetu wanaosema hawamtambui mufti hawana habari kuwa wakisema wamepata *registration,*basi ni mufti ndiye aliyekubali na kuweka saini yake.Kama si yeye basi wasingeipata.Sasa ni ajabu kumsikia mtoto akimwambia baba yake kuwa mimi sitaki kusikia maneno yako.

Kwa sheria ya nchi hii mpaka sasa ikiwa mufti atakwenda kuondosha mkono wake basi na nyinyi ndio basi.Ni nani anayeweza kusema kuwa mulipotaka kusajiliwa hamukuomba kupitia Bakwata?.Kama munakataa basi kataeni hapa ili watu wote wakusikieni. Tusiende mbali sana, kwa sababu mwisho mtu anaweza kuona ya nini kuzozana na watu ambao wasingekuwepo kama si mimi.

Tukitoka hapo naomba nirudie kwenye masuala yetu.

Kwa kuwa tunaheshimu wanazuoni wetu,hatupendi tukataja moja kwa moja kuwa fulani kasema kadha.Lakini mpaka leo hii bado naweza kusema kuwa kuna wanazuoni wanaoamini kuwa dunia imetandazwa kama jamvi,wanasema imeshikiliwa na pembe kubwa la ngo'mbe, akitingishika na dunia nayo inatingishika.Wengine wanasema kuna na chewa mkubwa sana kaka chini anaangaliana na chewa mwenzake,anasema ukitingishika naingia tumboni mwako.

Watu wenye mtazamo huu ukiwaambia kuwa mwezi ukichomoza unaandama kwa dunia nzima ndio mutaelewana,hawawezi kufahamu jambo jengine. Itikadi yao ni kuwa ukichomoza pembe yoyote ndio utaonekana kwa ulimwengu mzima na jua nalo pia likichomoza laonekana dunia nzima.Mmoja ya masheikh hao kaandika tafsiri yake siku za karibuni na ipo madukani hata hapa Dar es salaam.

Huyo bwana alifuatwa na sheikh mmoja kutoka Misri akamuuliza wee! bwana ndiye wewe unayesema dunia haizunguki,akajibu ndio! na kama ingekuwa kweli yazunguka basi waarabu siku moja wangekuwa Afrika na waafrika wakawa arabuni.Akamuuliza hivi; wewe umewahi kupanda ndege kwenda London au popote?.Akajibu nimepanda,akaulizwa hivi lile boeing likinguruma huko angani hukuona kuwa lilikuwa likiizunguka dunia?.Hakuwa na jibu lakini mpaka leo kitabu chake kiko hivyo hivyo,kuwa dunia haizunguki.

Watu wenye mawazo hayo wako tayari hata kuipindisha hadithi ili ikubaliane na mawazo yake ,kuwa mwezi ukiandama unaandama kwa dunia nzima.Hilo halishangazi.Wao hawaoni kuwa kuna uwezekano mwengine wowote ule.

Sasa nataka nizungumze hadithi za Mtume صلى الله عليه و سلم na tuone jinsi zinavyokubalika na wataalamu wa mambo ya falaki,na jinsi zilivyokaa sawa sawa sana.Hapo ndipo tutaona kwa nini tuna ***ikhtilaafu*** za ***mattaali'i***.Sio kwamba nimeambiwa na fulani na fulani ,ni hadithi zenyewe ndizo zinazotwambia.

Katika Qur'an imetajwa neno ***shahar***.Sheikh mmoja hapa hapa tumemsikia akiuliza:Hivi hii ***shahar*** ni kitu gani?.Bwana Mtume صلى الله عليه و سلم anatutafsiria yeye mwenyewe. Siku moja alipokuwa ametafautiana na ahli zake aliapa kuwa hataingia nyumbani kwa muda wa ***shahar***,halafu akaonekana baada siku 29 ataka kuingia nyumbani kwake.Mama Aisha akamuuliza;haa ! vipi bwana Mtume wataka kuingia nyumbani na wewe uliapa kuwa

hutaingia kwa muda wa ***shahar***.Akajibu kuwa ***shahar*** ni ***tis'a wa ishirini yawman***.Mara nyengine Mtume صلى الله عليه و سلم alipokuwa akieleza kusema kuwa sisi ni uma ambao hatujui kusoma wala kuhesabu,akaonesha mikono yake mara ya mwanzo akasema mwezi ni siku 30,mara ya pili akaonesha siku 29.

Hapa kafasiri ni siku 29 ,halafu kasema ni siku 30. Kama angelitaka si angesema tu tuhesabu siku 29 au 30 kisha tuanze kufunga.Tungelitengeneza kalenda tu kama wanavyofanya wenzetu na habari ingekuwa imekwisha. Lakini kwa sababu sisi hatuabudu ile sayari ndipo akasema kwa kauli nyengine;***swuumuu li ru'yatih***.Hii **ru'iya** ni kwa ajili ya ile ***hilaal*** kule juu .Nendeni kwenye tafsiri yoyote ile munayotaka muone,hii ina maana ya kuona tu.

Ndugu yangu pale alikuwa akijaribu kufasiri wanavyosema wanazuoni wa ***falaq***.Wanatafautiana kidogo,sio sana.***Manzila*** wengine wasema ziko 28 na wengine ziko 27 na masaa manane au tisa.Wanazuoni hao hao ambao wamesoma na elimu ya kiislamu halafu wakatugawia,wakasema miezi iko mitatu.Mwezi wa kwanza ni ***shahru haqiiqiy***,huu ni mwezi unaotoka pale unapoanza,ukaenda dauru mpaka pale pale ulipoanza.Huu unachukua siku 29 masaa 12 dakika 44 na sekunde 3.Hii ndio inakubaliana na mwezi aliosema Mtume صلى الله عليه و سلم .

Halafu kuna ***shahar islahiy***.Huu ni mwezi ambao kwanza unakuwa na siku 30 na unaofuata unakuwa na siku 29.Wanazuoni wa ***Falaq*** wanatwambia kuwa ***shahar islahiy*** mwezi wa kwanza 30,wa pili 29,wa tatu 30 wa nne 29 .Hivyo hivyo mpaka mwisho wa mwaka.Kwa utaratibu huu miaka yote huwa ni sawa sawa isipokuwa katika mwaka mkubwa mwezi wa mfunguo tatu ndio hubadilika kama hivi wanavyofanya wenzetu badala ya siku 29 unakuwa na siku 30.

Kwa hivyo utaona jinsi hadithi za Mtume صلى الله عليه و سلم zinavyokubaliana na huu uvumbuzi wa siku hizi.Hapo ndipo akasema fungeni kwa kuuona mwezi.Wanazuoni wote wa falaki wanataja miezi hiyo miwili,iwe ni ya kizungu au ya kiarabu hivyo ndivyo inavyokwenda.

Kuhangaika kuungalia mwezi ni ibada,ndio maana tukaambiwa fungeni kwa kuuona mwezi na fungueni kwa kuuona.Isingekuwa hivyo tungeambiwa tengenezeni kalenda tu.Mwenyezi Mungu ndiye aliyeuumba ulimwengu huu,na Mtume صلى الله عليه و سلم ndiye aliyekuwa akiteremshiwa wahyi.Mwenyezi Mungu anajuwa kabisa kuwa mwezi hauwezi kuonekana dunia nzima kwa wakati mmoja. Naye huwa haikalifishi nafsi.

Tunazungumzia kuuona mwezi, hatuzungumzii kupita ile sehemu yake iliyoanzia.Jamaa waliozungumzia falak wanasema ikipita ule muda wake siku 27 au 28 basi kwa muda wa masaa 24 huwa hauwezi kuonekana popote duniani.Mwezi unakuwa upo lakini hata ukitumia darubini huwezi kuuona ule mg'aro wa mwezi,labda kivuli chake tu.

Muda huo wa masaa 24 unapokuwa hauonekani ndio huitwa *birth of the moon.*Mwezi ukichomoza hapo ndiyo kalenda ya kiyahudi.Wataalamu wasema ni lazima yapite masaa si chini ya 20 ndipo uweze kuonekana.Ni lazima ile *reflection* ya jua iwe na nuru ya kutosha kuwezesha watu kuuona.

Kama utachukua darubini ukaangalia ukaona kitu kile chang'ara lakini ukiondoa darubini ikawa hukioni tena basi itakuwa bado hujafuata amri ya Mtume صلى الله عليه و سلم .Napenda kumuongezea ushahidi sheikh wangu alipokuwa akitoa hoja zake.Hapa kuna kalenda ya mwaka jana.Imetaja kwanza *location* (mahala),ikaandikwa *moon birth* na *moon age*.Mwisho ikaandikwa *visibility* na mwahala ambamo siku hiyo mwezi ungeonekana na mule ambamo usingeonekana.

La kushangaza ni kuwa *reference* ya Riyadh siku hiyo ya tarehe 9 Januari mwezi ulizaliwa, na moja kwa moja usingeweza kuonekana huko.Lakini siku hiyo hiyo mwezi ulitangazwa kuonekana Saudia.Hii ni kutoka huko huko kwa wataalamu.Ndipo pale mwenzangu aliposema kuwa mtindo huu wa Saudia haukuanza leo wala jana,ni zaidi ya miaka 25 tangu waanze kufuata kalenda ya kiyahudi.Kila siku sisi tunapotakiwa tuungalie mwezi ambapo tarehe ya kiislamu itaanza usiku, kwa wenzetu huwa kwao ni tarehe mosi.Lau kama wangekuwa wanakwenda kwa kuangalia mwezi wala lisingekuwa tatizo,mbona nchi chungu nzima zipo hapa mbona hakuna matatizo?.

Hawa ni wamarekani,lakini kuna wachina wote wainyooshea kidole Saudia, kwanini?.Mimi nakumbuka kuna mwaka mmoja alitoka mpakistani akaenda kuwaomba wasaudia wamuoneshe mtaalamu wao wa mambo ya mwezi,ajue imekuwaje umeandama kwao mara 4 kwa 29.

Nataraji mumenielewa.Masheikh wote najua munajuwa kuwa mwezi unakwenda kutoka magharibi kwenda mashariki,lakini wako wengine wanaosema kuwa watoka mashariki kwenda magharibi kwa kuifahamu sivyo ile aya ya 91:2 isemayo:***Na kwa mwezi unapolifuatia (jua)*** .Ukweli ni kuwa unatoka magharibi kwenda mashariki lakini unashindwa spidi na mzunguko wa dunia.Haya ninayoyazungumza ndilo shina la matatizo tuliyonayo.

- **HOJA ZA ANSAAR SUNNA**

Sheikh KASSIM HIMIID ABDULLAH MTARAWANJE

Mimi ndugu yenu naitwa Kassim Himiid Abdullah Mtarawanje,ni mwenyeji wa Kilwa na mkazi wa Dar es Salaam.

Nashukuru na mimi kupata nafasi kuchangia machache katika kikao chetu hiki ***adhwiim***.Ningependa kutanguliza machache yafuatayo.

Kwa kweli tupo kujadiliana kutafuta haki na hatupo hapa kutishana kuwa mtu atafuta chama au hatokifuta.Hilo ni hiyari ya mtu,hata akifuta chama naafute,lakini hatofuta itikadi nyoyoni kwa watu.Hapa tumekuja kuchangia ili kuona ni wapi kuna ukweli katika hoja ambazo sote tunazo.

Hakuna hata mmoja anayesema kuwa sisi twafunga kwa kufuata kalenda,wala kwa kuwafuata Saudia.Ikiwa Saudia wafunga kama tunavyofunga sisi ***wa bihaa neema***.

Kuhusu habari ya kuwa kwa muda wa miaka 25 Saudia wamekuwa wakifunga kwa kuwafuata mayahudi na kwamba hilo ndilo lililozaa ikhtilafu hizi.Hilo sio sahihi kwa sababu ikhtilafu hizi zipo tangu enzi za imamu Shaafiy,imam Malik na Ahmad bin Hambali na wengineo ***rahimahum Llaah***,ni mamia ya miaka wakati huo hata hakuna dalili ya kuwa kutakuwepo na Saudia.

Tuwache chuki za ***akhlaaqin shaqs***, kuchukia tu jambo.Tujadili lile mtu alilozungumza.Hakimu mzuri ni yule anayehoji hoja za yule aliyetuhumiwa.Tangu tumeanza kikao hiki wala hatujazungumza kuwa sisi tuko kwa ajili ya Saudia,wala hatujasema kuwa sisi ni ***Ansaaru mamlakatul arabiya***,sisi ni ***ansaaru sunna*** tu.Katika mamlaka yawezekana wako walevi ,wazinzi na kadhalika.Sisi hatuko kwa ajili ya kutetea hayo,bali kutetea suna tu kama jina letu lilnavyotuwakilisha.Kwa hivyo ndiyo maana siku zote hatujasema ***qaala Faisal, qaala Fahad*** au Khalid.Tunachosema sisi ni ***qaala Rasuulu Llaah swalla Llaahu alayhi wa sallam*** au ***qaala Shaafi'iyu***.Hayo ndiyo mazungumzo yetu kama mumetunakili vizuri.

Mwenyezi Mungu kasema katika suratul Maidah(5) aya ya 8:***Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutowafanyia uadilifu.Fanyeni uadilifu.Huko ndiko kunakowakurubisha na utawa.Na mcheni Mwenyezi Mungu.Hakika Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyafanya.***

Tuwe waadilifu juu ya tunayoyazungumza.Tuko juu ya masuala ya mwezi.Jee ni mwandamo mmoja au kila mmoja na wake ?.Mwenyewe mufti mwanzo kasema hapa kuwa tunajadiliana.Ikiwa sisi tumeswibu mutufuate,na ikiwa nyinyi mutaswibu tutawafuata.Nani anamsemea kweli mufti zaidi ya vile alivyosema mwenyewe?.Narudia,hatupo hapa kutishana na kufungiana vyama.

Lengo letu sote ni kutafuta pepo ya Mwenyezi Mungu.Wewe ukifunga kesho mimi nikafunga leo hakuna sisi tunachokipata.Lakini kwa kukuamrisha wewe kufanya baya na mimi nitakuwa napata dhambi.Muhimu ni sote tuonane ndugu na wala sio maadui.Tuitafute haki wapi iko?, si suala la baba na nwana, bali haki na baatili.Ikiwa hatukuifikia leo,tutaifikia siku nyengine.

Suala la swala ya Ijumaa na adhuhuri lilikuwa ni tatizo kubwa katika jamii yetu.Watu waligombana na kukosoana lakini hatimae limekwisha,hivyo hivyo kwa suala la khutba ya Ijumaa, iwe kwa kiarabu tu au kwa Kiswahili?,nalo pia lilmeeleweka.Hili la mwezi nalo litaeleweka.Zamani lilipoanza watu walidhani tafauti yetu na Saudia ni siku nzima.

Tumeelekeza mijadala yetu zaidi kwenye kuona,tumesahau kuwa kuna na kusikia na ni nyenzo muhimu aliyoitumia Mtume صلى الله عليه و سلم .Kwa kusikia hata ikiwa mufti hakutangaza basi wako watakaotangaza na watu watasikia.Hadithi sahihi juu ya hili ni ya bedui aliyekuja kwa Mtume صلى الله عليه و سلم akasema hakika mimi nimeuona mwezi.Mtume صلى الله عليه و سلم akamuuliza jee unamkubali Allah سبحانه وتعالى ,akasema naam.Akamuuliza na mimi nani?,akasema wewe ni Mtume wake.Akaamrishwa Bilal aadhini watu wafungue na waje waswali kesho.Hii ilikuwa nyakati za alasiri.Tutaona kuwa Mtume صلى الله عليه و سلم alikuwa haulizi wewe unatoka wapi?,na umbali gani.

Nilipokuwa nazungumza na sheikh Abdulrahman kuhusu hadithi hii,aliniambia kuwa bila shaka huyo bedui alikuwa akitoka maeneo ya jirani ambako unaweza kufika hata kwa punda.Akasema kilichozingatiwa hapo ni ukaribu.Nikamwambia ikiwa ni hivyo basi ni jambo la kushukuru,kwa sababu leo punda hawezi kutoka Dodoma akaja Dar es salaam kutoa habari ya kuandama mwezi.Ukitaka hivyo ni kuwa kila eneo na mwezi wao.

Hivyo muhimu lililozingatiwa ni taarifa tu.Kama kungekuwa na dharura nyengine yoyote basi Mtume صلى الله عليه و سلم pamoja na ujirani basi angeiuliza ili kuiarifisha.Hivyo ikabaki ni kuonekana kwa mwezi na hili sote tunakubaliana.Tofauti ni kuwa ni kuonekana kwa wote au kwa baadhi tu.Pili ni kupata habari na tatu kukamilisha siku 30 pindi mwezi haukuonekana na wala hazikupatikana habari juu ya kuonekana kwake.

Suala ya hadithi ya Kuraib kama ambavyo limesisitizwa sana.Hili suala linazihusu Damascus na Madina umbali wa takriban meli 850.Kwanza hakuna dalili kutoka kwa Mtume صلى الله عليه و سلم inayoonesha huo umbali ni mpaka kikomo gani.Ikiwa masafa haya yatakuwa ndiyo kigezo,maana yake ni kuwa mwezi ukiandama Mombasa kwa Mbeya ni zaidi ya masafa hayo.Sasa jee huku kutangaziana kwetu ni kufuata suna hiyo au ni kuikhalilfu?.

Tuangalie suala la mufti na ***biladil islam***.Hii Tanzania hakuna mtu anayeweza kusema ni nchi ya kiislamu.Kusema hivyo ni kutangaza kitu kisichokuwepo.Imeshasemwa kuwa nchi hii haina dini,lakini watu wake ndio wenye dini.Hivyo hakuna suala la kuwa na ***waliul***

amr.Masheikh akina sisi tunaweza kuwa mufti au mwenyekiti wa Bakwata,mwenyekiti wa Juwaquta au mwenyekiti wa Uvikita na kadahalika.

Namalizia na suala la katiba ya Bakwata.Mufti mwenyewe amefungwa na katiba yake akiwa ni mtekelezaji wa katiba hiyo.Katiba hiyo inatoa kibali kwa yeyote ambaye haridhiki na fatwa ya Bakwata akatafute fatwa pahala pengine.Bahati nzuri kuwa maneno ya mufti mwenyewe aliyoyasema yanathibitisha kuwa yeye anatekeleza hilo na hana mamlaka ya kulazimisha la akhera wala la dunia.Alipokuwa akizungumza alikuwa makini sana.Kama si hivyo basi angekwisha kuita dola akasema weka ndani wote hapa,na kikao hiki kisingekuwa na maana yoyote.

Suala la kalenda,hili limekaa katika vichwa vya baadhi yetu.Sisi hatufuati kalenda wala hatujazungumzia habari ya kalenda.Tunapoambiwa mwezi umeonekana kwa wapokezi ambao ni thiqa na kupitia njia zilizokuwa sahihi basi sisi tunafuata,si lazima iwe ni Saudia.Ukitaka kuhakikisha hilo basi ukiweza nenda mji wowote ukaandamishe mwezi halafu utangaze uone kama sisi hatutakufuata.Ni mara nyingi tu watu wamefunga kwa kufuata Philipines,na mara nyingi kwa kufuata Malaysia na nchi nyengine.

Sasa mathalan Saudia wameuona,ndio sisi tukatae !,kwani tuna ugomvi gani na Saudia?.Kwa haya nataraji tutakuwa tumeeleweka.

Wassalaam alaykum.

- **HOJA ZA BAKWATA**
  Sharifu HUSSEIN HASHIM

Mimi nataka kuzungumza kuhusu ilivyoulizwa,huko nyuma ilikuwaje?. Wakati wa Mtume صلى الله عليه و سلم waislamu walikuwa wakifungaje?.Kwa sababu kasoro zote hizi zimeanza takriban miaka 30 baada ya Mtume صلى الله عليه و سلم kuwa amekwisha fariki.

Ningependa kumalizia kikao hiki kwa kauli yangu binafsi,kwa kuangalia kitabu cha **KASHFUL GHUMMA AN JAMI IL UMMA**,kitabu cha sheikh Almawaaniy Abdulwahaab Al shaaraniy Almasry.Kasema hivi! katika ukurasa wa 192.***Kufaa kufunga siku ya shaka na kufaa kutumia machimbuko ya jua***:***Walikuwa maswahaba (Mwenyezi Mungu awawie radhi) hawawaamrishi watu walio mbali kufunga kwa kuonekana mwezi kwa watu wa miji mingine kama vile Madina.Maswahaba walikuwa hawaoni vibaya kwa watu wa miji mingine kutanguliza siku nzima juu watu wa miji mingine kwa kutumia ikhtilafu ya machimbuko ya jua.***

Narudi kule nyuma tulikotoka,tuliposema kuwa kila tutakavyozungumza kila mmoja atashikilia kauli yake.Kuna uchache na wingi,lakini wingi pia wazingatiwa katika sharia.Utawala nao vile vile wazingatiwa hata ukiwa ni wa kikafiri.

Paspoti utaipataje na watoaji ni makafiri?,makodi ya *income tax* utatoa na mahakamani tunakwenda hivyo hivyo.Tutafanyaje na ni dharura na dharura huyafanya mubaha mambo ambayo ni haramu !.

Mimi nikiwa ni msemaji wa mwisho,nasema kila tutakavyozungumza haitofikia kuwa hoja zetu na wenzetu hawa ikawa watazikubali.Kwa hivyo tufikie hapa tulipofikia.

Yupo mwenzetu mzee Matata ana yake machache tumsikilize na tusikie na mwenyekiti atasemaje.

Kabla kusimama sheikh Matata akasimama sheikh Issa Shaaban Simba akaomba naye apewe nafasi ya kuchangia aliyoikosa alipokuwa mwenyekiti.Kama kwamba upande wa Ansaar ulikuwa una hofu ya jambo wakapinga sheikh Issa kupatiwa nafasi

hiyo .Msemaji kutoka Ansaar akasema ikiwa ni wazungumzaji zaidi basi kila upande upate nafasi hiyo.Upande wa Bakwata ukasisitiza nafasi hizo zitolewe, lakini iwe ni zamu ya Ansaar kwanza kwa vile aliyemaliza alikuwa upande wao, ili sheikh Issa awe wa mwisho.Majibizano yakaendelea kwa muda,hatimae akaonekana skh Salim Msabah upande wa Ansaar akiendelea kuchangia.

- ***HOJA ZA ANSAAR SUNNA***
  Sheikh SALIM MSABAH

Sheikh wangu Hussein bin Hashim kasema suala la wengi linazingatiwa katika sheria lakini kwa bahati mbaya hakunukuu hata aya moja au hadithi au kauli yoyote ya mwanachuoni aliyesema kuwa wingi huzingatiwa.

Qur'an katika suratul Al An aam (6) aya ya 116 inasema :

Na ukiwatii wengi wa hawa waliomo duniani watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu.Hawafuati hawa ila dhana tu,na hawakuwa ila wasemao uongo tu.

Ushahidi mwengine ni pale Mtume صلى الله عليه و سلم alipowataka ushauri maswahaba juu ya mateka katika vita vya Badri.Walio wengi katika maswahaba walimshauri Mtume صلى الله عليه و سلم achukue vikomboleo.Wengine wakamshauri awatumie wale mateka katika kuwasomeshea waislamu.Sayyidna Omar pekee akataka mateka wale wauliwe.Ikateremka aya ya Qur'an ya 67 katika suratul Anfaal (8):

Haimfalii Nabii yeyote kuwa na mateka mpaka awe ameshinda barabara katika nchi.Mnataka vitu vya dunia ,na Mwenyezi Mungu anataka Akhera.Na Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu Mwenye hekima.

Wafasiri wengi wameitaja ***asbaabu nuzuul*** ya aya hii kuwa iliteremka kumuunga mkono sayyidna Omar ibn Khattab. Kwa maana hii, ndio tukasema hata demokrasia za nchi za magharibi si kwamba ndio njia za kupatia haki.Muhimu ni kuwa uamuzi wa walio wengi unaweza kuheshimiwa tu, lakini si msingi wa kukubalika kisheria.

Jengine imesemwa kuwa Salim;mimi na Salim Abdulrahiim wa Tanga kuwa ni watu wazuri na tumeikubali riwaya ya Kuraib.Hatujakataa kuwa riwaya hii ipo na imo kwenye Sahih Muslim.Lakini jamani kuwepo riwaya kwenye Sahihi Muslim haina maana kuwa riwaya hiyo ina maelezo unayoyakubali wewe.Hadithi sahihi,bali hata aya pamoja na usahihi wake,bado mtu anaweza akazielewa vibaya.

Mwenyezi Mungu سبحانه وتعالى kasema katika Qur'an;sura ya 3: aya ya 7:

Yeye ndiye aliyekuteremshia kitabu hiki.Ndani yake zimo aya 'muhkam' ambazo ndizo asili ya Kitabu (hiki).Na nyengine 'mutashaabihaat'.Basi wale ambao nyoyoni mna upotofu wanazifuata zinazofanana kwa kutafuta fitina…..

Miongoni mwa aya zenye mivutano miongoni mwa wanavyuoni ni aya hii.Ziko aya zenye kueleweka bila mjadala,na nyengine wanaingia watu matatizoni katika kuzielewa.Aya ya 187 katika suratul baqara inasema:

Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku..

Swahaba mmoja akachukua uzi mweusi na mweupe ili ajuwe wakati wa mwisho wa kula daku atakapoweza kuzitafautisha rangi za nyuzi hizo. Alipokwenda kwa Mtume صلى الله عليه و سلم akamfahamisha kuwa hayo sio makusudio ya aya.

Kwa upande wa riwaya ya Kuraib tunasema tena kuwa imo kwenye **Swahih Muslim**, lakini wanachuoni kadhaa wamesema haiwezi kutumika kama dalili kwa kuwa ina ***ihtimali***

nyingi.Wengine wasema ina kusudio hili,na wengine kusudio lile.Imam Suyuttiy ndivyo alivyosema alipokuwa akiisherehesha kwenye **Sunanu Nasaaiy**.

Wenzetu mara nyingi munatulazimisha kuifuata Saudia,naomba musitulazimishe hivyo.Kuhusu suala la matlai wako wanachuoni wa zamani na sasa wanaoyakataa kutumika.Ama kuhusu waislamu walio wachache katika nchi, kuwa ndio wanaofaa kutumia muandamo wa nchi nyengine na kwamba katika nchi ambako waislamu ni wengi ni lazima wafuate muandamo wao.Bahati mbaya wenzetu hamjanakili dalili kutoka katika kitabu chochote chenye kusema hilo.

Wakati sheikh Salim akihitimisha kwa kujaribu kufafanua hadithi ya Mtume صلى الله عليه و سلم ***'sisi ni umma ambao hatujui kusoma wala kuhesabu' mkanda,sehemu uliyorekodiwa ukakakata.Kwa mtazamaji na msomaji wa mjadala huu hapo ndio mwisho.***

Wassalaam alaykum warahmatu Llaah.

.....

Umalizapo kusoma mjadala huu tuma kura yako juu ya nani aliyeshinda kwa hoja, kati ya Bakwata na Ansaar Sunna.Kila baada ya muda apendandapo Allah سبحانه وتعالى ***tutakuwa tukichapisha matokeo.Tuma kura yako kupitia*** ***uongofu@islamicalendartides.com***